# Nipashe

Jumatatu Januari 13, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580126

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710





UKURASA 13



## Profesa aona tatizo kasi ongezeko la watu nchini

UKURASA 4

# Marufuku ujenzi wa nyumba bila kibali

**NI** maeneo yote ya mijini, waziri afunguka kuhusu utaratibu mzima kuwa...

*Endelea ukurasa wa 2*



## SHEIN ADOKEZA ONGEZEKO MISHAHARA

UKURASA 2

Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akikagua gwaride maalum la Maadhimisho ya Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Uwanja wa Amaan Zanzibar jana.
**PICHA: IKULU**


Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


## Chadema sasa yapania majimbo Dodoma 2020

UKURASA 3


**MICHEZO** | **SIMBA: NI KOMBE TU** UK. 32 | **MAONI, KATUNI UK.6**

## Madiwani washtuka kisa msako wa polisi

**Na Mwandishi Wetu**

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge wameiomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora kuchunguza nia ya polisi kutoka mkoani kwenda katika Kijiji cha Mpombwe na kuanza kuchukua bidhaa kwenye maduka bila Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Sikonge kuwa na taarifa.

Ombi hilo la madiwani lilitolewa jana baada ya Diwani wa Kata ya Mpombwe, Juma Mdulla, kueleza tukio lililotokea Januari 8, mwaka huu katika kijiji hicho wakati akichangia hoja kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani la Sikonge ya kujadili na kupitia mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya mwaka 2020/21.

Alisema Polisi kutoka Tabora Mjini walifika katika kijiji hicho na kwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji kumtaka awaongoze kuendesha ukaguzi bidhaa zilizokwisha muda wake kwenye maduka yaliyopo eneo hilo.

Diwani huyo alisema chakusikitisha walifanya kazi hiyo wakiwa pekee yao bila hata kuwa na wataalamu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na viongozi wengine kama wataalamu wa sekta ya afya na mtendaji wa kata.

Aliongeza kuwa katika ukaguzi huyo, walichukua baadhi ya vipodozi na mafuta ya petroli, jambo ambalo liliacha maswali mengi.

Mdulla alisema kuwa alipojaribu kufuatilia juu ya taarifa za uwapo wa zoezi hilo, hakupata majibu, lakini alibaini kuwa askari hao walifika na kuanza kazi bila hata kutoa taarifa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge wala hawakusaini kitabu cha wageni cha kijiji hicho, jambo ambalo limeacha maswali kama kweli askari hao walikuwa kazini au walikuwa katika shughuli zisizo halali.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Peter Nzalalila, alisema kitendo kilichofanywa na askari hao hata kama kilikuwa halali, lakini walipaswa watoe taarifa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na kuongeza kuwa vema Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala Mkoa wakapelekewa taarifa hiyo ambayo imewasikitishwa.

Alisema kumezuka tabia ya taasisi mbalimbali kuingia katika Wilaya ya Sikonge na kuendesha shughuli zao na wakati mwingine kuwabughudhi wananchi bila hata kutoa taarifa kwa mamlaka ya juu za wilaya ikiwamo kwa Kamati ya Usalama ya Wilaya.

Kwa upande wa Katibu Tawala Wilaya ya Sikonge, Renatus Mahimbali, alisema utaratibu unataka kabla ya taasisi yoyote haijaanza kazi yake ionyeshe vibali vinavyowataka kufanyakazi hiyo na watoe taarifa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Alisema watu wanaoingia Sikonge na kuendesha shughuli zao bila Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuwa na taarifa watachukuliwa kama wahalifu.

Alitoa mfano hivi karibuni alipata taarifa kutoka kwa wananchi ya kuwapo na watu wanaodai kuandikisha wastaafu na alipojaribu kuwahoji kwa njia ya simu na walipobaini kuwa ni utapeli wao umegundulika walikata simu na kuondoka.

Aliwaomba madiwani kuhakikisha kuwa wanapoona wageni wanaendesha shughuli katika maeneo yao wawaombe vibali vinavyowapa ruhusa ya kufanyakazi hiyo.

# Marufuku ujenzi bila kibali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imepiga marufuku shughuli zozote za ujenzi kufanyika maeneo ya mijini bila kuwa na kibali, huku kukiwa na tishio la kubomoa nyumba zilizojengwa pasipo vibali vya mamlaka husika.

Onyo hilo lilitolewa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alipokuwa akizungumza na wananchi wa mtaa wa Ndachi Kata ya Mnadani katika ziara yake ya kutembelea eneo hilo na eneo la Nkuhungu Broad Acer, jijini Dodoma.

Akikagua nyumba zilizojengwa kwenye eneo hilo bila vibali, alisema jambo hilo halitakubalika na sheria inaruhusu kubomoa nyumba za aina hiyo.

Aidha, waziri huyo aliweka alama ya X kwenye nyumba ambazo wamiliki wa viwanja wameanza ujenzi bila kuwa na vibali kutoka Ofisi ya Ardhi ya jiji hilo, na kuamuru kusitisha ujenzi huo.

Akiwa katika eneo hilo alimpigia mmoja wa wamiliki ambaye ni mtumishi wa umma ambaye mafundi walikutwa wakiendelea na ujenzi bila vibali.

"Ninataka nione hati yako, kibali cha ujenzi, unajua mtumishi wa umma hujengi mahali hadi uwe umemiliki na kupewa kibali cha ujenzi na Manispaa, kwanini umeamrisha pajengwe," alihoji.

"Samahani waliniambia huku hawana vibali kwa kuwa ni pembezoni mwa mji," alijibu dada huyo na waziri kusema: "Sheria haijasema pembezoni mwa mji watu wajenge tu, sasa usiendelee kujenga nasimamisha leo, mwambie fundi wako aache kujenga na ujenzi hadi upate kibali."

Akizungumza na wananchi hao, alisema: "Mtu yeyote anayejenga mjini mahali popote bila kufuata utaratibu wa kumilikishwa yaani kiwanja ambacho hakijapimwa, hujamilikishwa, huna kibali cha wenye mamlaka ya mji unaohusika ujue unajipeleka kwenye hatari ya kuvunjiwa na kuondolewa jengo lako."

"Msinijaribu na msimjaribu Mahenge (Mkuu wa Mkoa wa Dodoma), sisi serikali tuna nguvu, ole wenu tukute vyoo vinajengwa, mapagale yanajengwa tutayavunja, tumeshavumilia vya kutosha," alisema.

Kwa mujibu wa Lukuvi, kila anayejenga hata kama ana pagale au msingi serikali itatafuta namna ya kumilikisha, na kwamba kwa sasa wanatakiwa kuacha wapime zipatikane barabara, viwanja vya watoto na ndipo umilikishaji uendane na ukubwa wa viwanja, na ujenzi waanze baada ya kupata vibali.

"Urasimishaji unaofanyika sasa ni huruma ya Rais, lakini kwa sheria ilitakiwa ni marufuku kuwabariki watu waliojenga kwa kuvunja sheria bila vibali, Rais aliniagiza waliotoa jasho lao wakajenga mjini wasivunjiwe ndiyo maana tunarasimisha makazi," alisema.

Aidha, Waziri Lukuvi alisema serikali haina mpango wa kubomoa nyumba za wananchi isipokuwa wanatakiwa kujenga kwa kufuata utaratibu ikiwa ni pamoja na kupata kibali cha ujenzi.

Wakati huo huo, Waziri Lukuvi amefanikiwa kutatua mgogoro wa ardhi kwa wakazi wa Ndachi

INAENDELEA UK.8



Makomandoo wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wakionyesha ukakamavu wao, wakati wakipita mbele ya jukwaa kuu na kutoa heshima kwa Rais wa Zanzibar katika sherehe za Miaka 56 ya Mapinduzi zilizofanyika jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Shein adokeza ongezeko mishahara

**Na Waandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kutokana na kuongezeka ukusanyaji wa mapato ya serikali, watumishi wasishangae kuongezewa mishahara.

Pia amesema ataendelea kushirikiana kikamilifu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli, kuhakikisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unadumu ili nchi iendelee kuwa na amani.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati wa sherehe za maadhimisho ya Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, vyama vya siasa, taasisi na wananchi kutoka Bara na Visiwani.

Hata hivyo, Dk. Shaun hakutoa maelezo zaidi kuhusiana na uwezekano wa watumishi wa umma kuongezwa mshahara.

"Niwahakikishie tu kwamba muungano wetu utaendelea kudumu, mimi na Rais John Magufuli tutaendelea kutekeleza wajibu wetu wa kikatiba na kisheria katika kulinda amani na utulivu wa wananchi pamoja na mali zao na hatutochelea kumchukulia hatua mtu yoyote yule atakayejaribu kuhatarisha amani ya nchi," alisema Rais Shein.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria ni Rais Magufuli, marais wastaafu Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete na Amani Abeid Karume pamoja na mawaziri wakuu wastaafu wakiwamo Edward Lowassa, Frederick Sumaye na Mizengo Pinda.

Wengine ni Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, mawaziri na viongozi wa vyama vya siasa akiwamo Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba.

Katika sherehe hizo, Rais Shein alitaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika

INAENDELEA UK.8

HABARI KITAIFA

# Watumishi ardhi wabanwa kujieleza

Na Munir Shemweta,
NJOMBE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ameagiza wakuu wote wa Idara za Ardhi, Halmashauri za Mkoa wa Njombe kuandikiwa barua za kujieleza kutokana na kushindwa kusimamia uingizaji taarifa za viwanja kwenye mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji kodi ya serikali.

Aidha, alitoa miezi mitatu kuanzia Januari 11, hadi Aprili 12, mwaka huu, kwa halmashauri za mkoa wa Njombe kumpatia taarifa ya kuingizwa viwanja vyote vya wamiliki wa ardhi kwenye mfumo wa kielektroniki katika mkoa huo.

Mabula alitoa agizo hilo jana katika kikao chake na watendaji wa sekta ya ardhi wa halmashauri sita za mkoa wa Njombe akiwa katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi pamoja na kukagua miradi ya ujenzi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Wakuu wa idara ya ardhi walioangukia mikono ya Mabula kuhusiana na kuandika barua za kujieleza ni kutoka Halmashauri za Njombe Mji iliyoingiza viwanja 7,301, Makambako 5,712, Njombe Wilaya 326, Wanging'ombe 375, Makete 2,156 na Ludewa viwanja 3,793.

Uamuzi wa Naibu Waziri unafuatia kuelezwa kupitia taarifa ya mkoa wa Njombe pamoja na zile za halmashauri zote za mkoa huo kuwa, kuanzia kipindi cha Julai hadi Desemba 2019 ni viwanja 19,645 tu ndivyo vilivyoingizwa kwenye mfumo kati ya viwanja 40,961.

Kwa mujibu wa waziri huyo, utaratibu wa kuingiza viwanja kwenye mfumo wa kielektroniki ulianza mwaka 2017, lakini cha kushangaza hadi kufikia sasa zipo baadhi ya halmashauri hazijaunganishwa.

Alisema, kuingiza viwanja kwenye mfumo wa kielektroniki siyo tu unarahisisha kutambua wamiliki

INAENDELEA UK.8

# Chadema yamezea mate majimbo Dodoma

Na Renatha Msungu,
DODOMA

MWENYEKITI wa Kanda ya Kati wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Lazaro Nyalandu, amesema moja ya zawadi ambayo wanataka kuwapa wanachama wao ni kushinda viti vyote vya ubunge Mkoa wa Dodoma.

Aidha, amesema anatambua kuwa mkoa huo hauna historia ya wabunge wa upinzani kushinda ili kuishangaza CCM katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Nyalandu ambaye amewahi kuwa waziri na mbunge katika serikali ya awamu ya nne, ameiomba serikali kuhakikisha kuna kuwa na tume huru ya uchaguzi ili kila chama kishinde kwa haki, na si kurudia mambo yaliyofanywa katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, Nyalandu alisema moja ya mikakati Chadema iliyojiwekea ni kuhakikisha wanashinda makao makuu ambapo viongozi wote wa chama tawala na serikali wapo.

Alisema moja ya mbinu ambazo watazitumia ni kuwa na wanachama wengi, na kwamba wameshawaandikisha watu wao wote katika daftari la kudumu la wapigakura.

"Kuna njia nyingi ambazo tutatumia ili tushinde uchaguzi ujao... hatuwezi kuzisema zote kwa sababu tutawarahisishia wapinzani wetu CCM," alisema Nyalandu.

Alisema Dodoma ni kubwa, lakini kwa mikakati waliyopanga lazima washinde kwa kishindo, huku wakiwataka CCM kutohofia chochote bali wakutane ulingoni kugombea viti mbalimbali katika uchaguzi huo.

"Naviomba vyombo vya ulinzi na usalama visiingilie mambo ya siasa, wao wafanye kazi yao nasi tutaheshimu sheria za nchi zilizowekwa, hakuna atakayekwenda kinyume," alisema Nyalandu.

Alisema Chadema imejipanga kuichukua Dodoma kwa sababu ni sehemu ya mkakati waliojiwekea.

"Tulitembea nyumba hadi nyumba eneo la Ikoje, huku tukiwasemesha Kinyaturu, lakini baada ya matokeo tulipigwa na kupoteza lile jimbo," alisema Nyalandu.

Akizunguzia suala la kuhamia Chadema, Nyalandu, alisema alikaa nalo mwaka mmoja ndipo siku moja alimwambia mke wake ambaye alishtuka na kushangazwa na uamuzi huo.

"Naomba niwaambie kuhama kwangu CCM sio upepo wa kisulisuli, mafuriko wala nguvu ya soda bali hii ni nguvu ya 'wine', kadri siku zinavyoendelea ndio inazidi kuwa bora nami sibahatishi, nimedhamiria," alieleza.

**MIKOPO ELIMU YA JUU**

Akizungumzia suala la elimu kwa ujumla, alisema serikali inapaswa kubadilisha mfumo haraka kwani unawagharimu sana wanafunzi wa elimu ya juu hususani suala la mikopo.

"Haiwezekani mwanafunzi anadai haki yake ya mkopo unamsimamisha chuo au kumfukuza hiyo roho ya ukatili Tanzania haipo mweleweshe, lakini kumtoa chuo unamwaharibia malengo na hujui watu wangapi wako nyuma yake wanamtegemea," alisema Nyalandu.



RIPOTI MAALUM

# Profesa aona tatizo kasi ongezeko la watu nchini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TOVUTI rasmi ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaonyesha Tanzania kwa sasa inakadiriwa kuwa na watu 55,890,747. Kati yao, wanaume ni 27,356,189 na wanawake 28,534,558.

Kwa makadirio hayo, idadi imeongezeka kwa watu milioni 43.59 katika kipindi cha miaka 42 kwa kuwa takwimu za NBS zinaonyesha mwaka 1967 (sensa ya watu ya kwanza nchini), Tanzania ilikuwa na watu milioni 12.3, Tanzania Bara ikiwa na watu milioni 11.9 na Zanzibar watu 354,815.

Huku kukiwa na kasi hiyo ya ongezeko la watu, nchi iko katika safari ya kuelekea uchumi wa kati na mada kuu katika safari hiyo ni ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Juni 1999, Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kupunguza nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Wakati safari hiyo ikiwa imeiva, Kamishna Mhifadhi wa Misitu wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Profesa Dos Santos Silayo, anaungana na wadau wengine wanaopaza sauti kuhusu kutoka maeneo tofauti ya kitaifa kuhusu madhara ya kasi ya ongezeko la watu nchini.

Mbali na Profesa Silayo, wadau wengine 'wanaolia' na kasi ya ongezeko la watu nchini ni pamoja na Rais mstaafu wa awamu ya nne, Benjamini Mkapa, ambaye katika kitabu chake cha 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Kusudio Langu), anaeleza kile anachokiona nchi kukosa dira sahihi ya kukabiliana na tatizo hilo.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dodoma wiki iliyopita, Profesa Silayo alielekeza kilio chake kwa baadhi ya watu wanaosaka maeneo mapya na kuelekeza nguvu zao kwenye kuvamia na kubadili matumizi ya maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za uhifadhi, hasa misitu na mapori tengefu.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na Mtendaji Mkuu huyo wa TFS:-



Kamishna Mhifadhi Misitu wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo

**SWALI: Vipo vilio vya wadau wa uhifadhi na utalii dhidi ya kasi ya ongezeko la watu nchini. TFS mnaichukuliaje kasi hii?**

**PROFESA SILAYO:** Moja ya vikwazo kwetu ni kasi ya ongezeko la watu ukizingatia idadi kubwa ya watu nchini hupenda kutumia nishati itokanayo na mimea kama mkaa, kuni na vitu mbalimbali.

Hili linatupa mtihani mkubwa kutokana na kwamba inahitajika elimu kwa wananchi ili kuepuka kukata miti na kufyeka misitu ovyo, vinginevyo kutasababisha jangwa hapo baadaye.

Ukataji miti unatokana na baadhi ya watu kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana na utunzaji bora rasilimali za misitu zilizopo nchini.

Sasa, panapokuwa na mtawanyiko wa watu, moja kwa moja panachangia uvamizi wa hifadhi za misitu na kusababisha uharibifu mkubwa.

Kukishakuwa na mtawanyiko mkubwa, shughuli za ufugaji zinaleta uvamizi, shughili za kilimo zinachangia kukata misitu ovyo, kunakuwa matatizo makubwa ya uharibifu wa hifadhi za misitu.

**SWALI: TFS inachukua hatua zipi kuhakikisha kasi ya ongezeko la watu nchini haisababishi kuwa na Tanzania isiyo na misitu?**

**PROFESA SILAYO:** Mikakati iliyopo ni pamoja na kutoa elimu kwa vijiji 150 kuhusu utunzaji na matumizi bora ya ardhi. Tunaamini kwa kufanya hivi, itasaidia kwa kiasi kikubwa jamii kujua umuhimu wa hifadhi ya misitu iliopo nchini.

Mkakati huu umelenga kupunguza matumizi mabaya ya hifadhi za misitu ambayo ina manufaa makubwa katika kuhakikisha uchumi wa nchi na afya za binadamu kutokana na uzalishaji wa hewa safi.

Maeneo ambayo bado hayajapangwa, yanakuwa na ugumu katika kuyasimamia kutokana na mtawanyiko wa watu katika eneo husika.

**SWALI: Kwa kasi hii ya ukataji miti, Tanzania itakuwa na misitu katika miaka 100 ijayo?**

**PROFESA SILAYO:** Ili nchi iwe na misitu miaka 100 ijayo, kila mmoja anapaswa kuwa askari wa wenzake katika kuihifadhi na kuilinda, kwa sababu hifadhi za misitu zinahitaji matunzo bora ili ziendelee kushamiri.

Kila mmoja ana haki ya kuitunza misitu vizuri, kwa sababu ni mali yetu wenyewe. Ndiyo maana nasisitiza kila mmoja ni mlinzi wa hifadhi za misitu zilizopo nchini.

Misitu ikitunzwa, ina faida nyingi sana kuliko watu wanavyofikiria. Moja, ikitunzwa inaleta hewa safi, maji yatapatikana kwa wingi na vitu vingine mbalimbali vinavyosababishwa na uwapo wa misitu bora yenye afya nzuri.

Ili tuendelee kuwa na hifadhi nchini, serikali inapaswa kuanzisha miradi ya maendeleo ambayo wananchi wanaweza kuitumia kufanya maendeleo bila kuathiri hifadhi za misitu zilizopo nchini.

Miradi hiyo ikiwapo na wananchi wakipewa elimu jinsi ya kuitumia, hakuna atakayekata miti na kufyeka misitu ovyo, bila kusahau kwamba zinahitajika jitihada kukabiliana na mtawanyiko wa watu ambao nimeeleza awali kuwa ni chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira ya hifadhi za misitu zilizopo.

Kwa hiyo, nchi lazima iwe na mikakati ya kuwajengea wananchi maisha bila kutegemea misitu iliopo. Tukumbuke idadi kuwa ya wananchi wanatumia nishati ya kuni na mkaa katika kupikia.

Misitu yetu tukiilinda, itaendelea kuleta faida kubwa. Misitu inaleta tiba na vitu vingine vingi ambavyo vinatokana na uwapo wake.

Pia, kuna kila sababu serikali kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji na kilimo ili wakulima na wafugaji kila upande uwe na mipaka yake.

Tumeuanza mwaka wa tano wa uongozi wa serikali ya awamu ya tano. TFS inajivunia nini katika uongozi wa serikali hii?

**PROFESA SILAYO:** Tunajivunia kuanzisha viwanda vingi vikubwa vinavyotegemea rasilimali za misitu ambavyo vina uwezo wa kuzalisha bidhaa bora kwa matumizi ya wananchi.

Kwa mfano, sasa nguzo bora za umeme zinapatikana nchini. Kuna viwanda vinavyotengeneza nguzo zenye uwezo wa kudumu miaka hamsini. Kuna viwanda vya misitu vimeboreshwa ambavyo vinaleta faida kubwa, ikiwa ni pamoja na kuchangia kuingiza mapato ya nchi kupitia utalii.

Awali ilikuwa idara ya misitu na wafadhili walikuwapo lakini vitu vingi walifanya kwa manufaa yao tofauti na ilivyo sasa, tunafanya kwa faida yetu.

Hivi sasa misitu inasaidia uzalishaji wa samaki kutokana na maji yaliyopo. Utunzaji na ulinzi wa misitu umechangia kuwa na uhakika wa maji nchini.

Suala usalama liko vizuri kabisa hasa ukizingatia ndani ya miaka minne, tumeweza kubadilisha kutoka uendeshaji wa kawaida na kuwa Jeshi Usu, imesaidia kwa kiasi kikubwa sana kuimarisha ulinzi na usalama wa hifadhi za misitu yetu.

Tuna kila sababu ya kuishukuru serikali ya awamu ya tano kwa sababu hivi sasa TFS ina uwezo wa kununua magari 35 kila mwaka na mitambo yake, hilo si jambo dogo wakati awali ilikuwa magari 10 tu.

Usafiri umeimarika kuanzia ngazi ya chini hadi juu na utendaji kazi umekuwa rahisi sana. Kwa kweli tunapaswa kujivunia kutokana na serikali hii.

Kwa upande wa mistu iliyo kisiwani, tuna boti ambazo zina uwezo wa kufanya doria ndani ya bahari ili kudhibiti wahalifu wa misitu. Pia, tumefanikiwa kupandisha hadhi ya misitu tisa, hilo siyo jambo dogo kabisa katika maendeleo.

Misitu mingi ilikuwa na migogoro, lakini tumefanikiwa kuitatua na jamii ya maeneo hayo sasa inatuamini na tunashirikiana nayo katika kutunza hifadhi za misitu mbalimbali iliyopo nchini.


**SWALI: TFS inakabiliwa na vikwazo vipi vikubwa kwa sasa katika utekelezaji wa majukumu yake ya kisheria?**

**PROFESA SILAYO:** Kikwazo kikubwa ni uvamizi wa misitu unaofanywa na jamii inayozunguka misitu, lakini kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kuidhibiti kwa sababu moja ya mkakati tulioujiwekea ni kutoa elimu vijijini na mkakati tulionao sasa ni kuanza na vijiji 150 halafu tutaendelea na vingine.

Tukishakamilisha utoaji wa elimu kwa jamii, tutakuwa na uhakika wa ulinzi wa hifadhi zetu kwa sababu kila mmoja atakuwa mlinzi wa mwenzake.

Katika kutoa elimu kwa jamii, tumekuwa tukiwasaidia wananchi kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inasaidia kuepusha matumizi mabaya ya misitu.

Ningependa kila mwananchi atumie zaidi gesi na umeme kama mbadala wa kuni na mkaa, ili kuacha kukata miti ovyo. Ifike wakati hifadhi za misitu ziwe za kwanza katika fikra zetu za ulinzi kabla ya kufikia mambo mengine.




**SENSA TANZANIA**

| Mwaka | Idadi ya watu | Tanzania Bara | Zanzibar |
|---|---|---|---|
| 1967 | 12,313,469 | 11,958,654 | 354,815 |
| 1978 | 17,512,610 | 17,512,610 | 476,111 |
| 1988 | 23,095,878 | 22,455,193 | 640,685 |
| 2002 | 34,569,232 | 33,584,607 | 984,625 |
| 2012 | 44,928,923 | 43,625,354 | 1,303,569 |

**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).**

# Mnyika ataka mabadiliko ya Katiba mkutano ujao Bunge

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), John Mnyika, ametaja maeneo manne ya kwenye Katiba yanayohitaji marekebisho.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema ipo haja kwa Rais John Magufuli kupeleka marekebisho ya katiba kwenye kikao cha bunge kinachotarajiwa kuanza Januari 28, mwaka huu.

Alitaja maeneo hayo kuwa ni kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi, matokeo ya uchaguzi wa Rais kupingwa mahakamani, mgombea urais kupata zaidi ya asilimia 50 (50%+1) na wagombea wa nafasi za ubunge na udiwani kupigiwa kura ya ndiyo au hapana inapotokea kuna mgombea mmoja, badala ya sasa ambapo hupita bila kupingwa.

Kwa mujibu wa Mnyika, marekebisho hayo yatakuwa mwarobaini wa kuepusha uhasama, vurugu na mtanziko wa kisiasa unaotokana na kuvurugwa kwa uchaguzi nchini, kama ilivyotokea Zanzibar mwaka 2015.

Mnyika ambaye ni Mbunge wa Ubungo, alisema maeneo muhimu yanayohusu uchaguzi ili wapigakura, wapate fursa ya kuchagua viongozi bora kupitia sanduku la kura kwa ajili ya maendeleo ya wote.

Aidha, Katibu Mkuu huyo alitoa maagizo kwa wabunge wa Chadema kwa kushirikiana na wabunge wengine wa upinzani bungeni kuhakikisha kuwa agenda ya marekebisho ya uchaguzi inapewa uzito na kipaumbele kwenye mkutano wa 18.

Alisema mchakato huo uanzie kwenye vikao vya Kamati za Bunge ambavyo vimepangwa kuanza vikao vyake Januari 13, mwaka huu, huku vikao vya Bunge zima vikipangwa kuanza Januari 28, mwaka huu.

Katibu Mkuu Mnyika alisema maeneo ambayo Katiba inapaswa kufanyiwa marekebisho ya haraka kukidhi matakwa na maslahi ya Watanzania wakati taifa linaelekea kufanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ili kuhakikisha kuwa haki ya wapigakura kuchagua viongozi bora wanaowataka haipokwi wala kuchezewa.

"Mswada huo wa marekebisho ya Katiba ulenge kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, uchaguzi wa urais kupingwa mahakamani, mgombea urais kushinda kwa kupata kura zaidi ya asilimia 50 na wagombea wa nafasi za ubunge na udiwani kupigiwa kura za ndiyo au hapana kama ilivyo kwa mgombea wa urais," alisema na kuongeza:

"Inapotokea kuwa mgombea wa ubunge au udiwani yuko peke yake. Tusiruhusu masuala ya watu kupita bila kupingwa ambayo ndiyo yanawasaidia wakurugenzi na wasimamizi wa uchaguzi kukimbia ofisi kukwepa kuteua wagombea wa upinzani."

Aidha, alisisitiza kuhusu tume huru ya uchaguzi nchini, amesema kuwa umuhimu wa suala hilo si kwa ajili ya vyama vya siasa pekee, hivyo ametoa wito kwa wadau wengine, asasi za kiraia nchini, madhehebu na viongozi wa dini nchini na makundi mengine mbalimbali nchini kuungana katika jambo.



Mwonekano wa daraja la Mto Msia katika Kijiji cha Msia, ambalo limekata mawasiliano baina ya wananchi wanaotokea mkoa wa Songwe kuingia Mkoa wa Rukwa na kuelekea Katavi kutokana na mvua kubwa zilizonyesha. **PICHA: OFISI YA MKUU WA MKOA RUKWA**

# Fursa pembejeo bure wazee miaka 60

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZEE wenye umri wa miaka 60 na kuendelea katika kijiji cha Wisolele Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wamepatiwa zana za kilimo na pembejeo bure kwa ajili ya maandalizi ya kilimo.

Pembejeo hizo zinatolewa na uongozi wa mgodi mdogo wa pamoja Gold Mining Rush.

Akikabidhi vifaa hivyo jana, Mwenyekiti wa Mgodi huo, Hamisi Mabubu, kwa wazee 60 wanaozunguka mgodi, alisema wazee wengi katika kijiji cha Wisolele wanashindwa kulima mashamba kutokana na changamoto ya pembejeo na zana za kilimo.

Alisema kuwa ugawaji wa zana za kilimo na pembejeo utakuwa unafanyika kila mwaka hasa kwa wazee wenye umri wa kuanzia miaka 60, na kwamba kila mzee aliyepatiwa pembejeo ahakikishe analima na sio kuuza. Pembejeo hizo ni majembe, mbegu za mahindi ikiwamo mbegu za alizeti, mbolea za kukuzia na kupandia vyote vikiwa vimegharimu kiasi cha Sh. milioni 1.5. "Wazee wetu wana maeneo makubwa ya kilimo, lakini hawana uwezo wa kununua zana za kilimo na pembejeo, na sisi kama viongozi wa mgodi tumeliona hili na kuchukua maamuzi ya kugawa pembejeo, mbegu na zana za kilimo bure kwa wazee wanaozunguka mgodi," alisema.

Lucas Shija, mzee wa kijiji cha Wisolele, alishukuru uongozi wa mgodi kuwapatia pembejeo na zana za kilimo bure na kudai kuwa alikuwa ameshakata tamaa ya kuendelea kulima maeneo yake baada ya kukosa pembejeo za kilimo.

## Bangi yampeleka jela kwa kushindwa kulipa mil. 1.7/-

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi imemuhukumu mkazi wa Kijiji na Kata ya Mandawa, Wilaya ya Kilwa, Hamisi Mohamedi Mtungata (30), kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. milioni 1.7 kwa kosa la kumiliki na kusafirisha bangi kilo 14.89.

Hukumu hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Mnyonga Magala, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na pande zote.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Magala alimuuliza mshtakiwa kama ana sababu za msingi kutokana na kosa linalomkabili, ambaye aliiomba asipewe adhabu kali kwani ni mkosaji wa kwanza, pia ana familia mke na watoto wawili wanaomtegemea.

Baada ya utetezi huo, Mahakama hiyo alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba kama ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hana.

Aidha, aliomba mshtakiwa apewe adhabu kali kulingana na kosa alilolifanya hasa ikizingatia dawa za kulevya zimekuwa zikiharibu akili za wananchi kwenye jamii.

Hakimu Magala akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 20/2019, kwa kumtaka mshtakiwa huyo kulipa faini ya Sh. milioni 1.7 na akishindwa atumikie kifungo cha miaka mitatu Gerezani.

Hata hivyo, mshtakiwa Mtungata, alishindwa kulipa faini, na kwenda jela kutumikia adhabu hiyo.

Awali, Mramba, aliiambia mahakama hiyo kuwa mshtakiwa alikamatwa Machi 15, mwaka 2019, na askari Polisi wa Usalama Barabarani waliokuwa eneo la Mitwero akisafirisha bangi hiyo kwenye basi la Kampuni ya Warder lenye namba za usajili T 997 DPL akitokea Mtama kwenda Dar es Salaam.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Mtibwa burudani itawale fainali Mapinduzi

**BAADA** ya jana wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla kusherehekea Miaka 56 ya Mapinduzi, leo watahitimisha sherehe hizo kwa kushuhudia mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi kati ya Simba na Mtibwa Sugar.

Timu hizo zote kutoka Tanzania Bara, zinashuka dimbani baada ya safari ndefu kuanzia hatua ya mtoano, nusu fainali na hatimaye fainali itakayopigwa Uwanja wa Amaan kuanzia saa 2:15 usiku.

Mtibwa Sugar imefika hatua hiyo kwa mikwaju ya penalti katika mechi zake zote ilizocheza kwenye mashindano hayo mwaka huu.

Ilianza kwa kuitoa Chipukizi kwa penalti 4-2 baada ya sare ya bao 1-1 kwenye hatua ya mtoano kabla ya nusu fainali kuitupa nje Yanga kwa idadi kama hiyo ya penalti kufuatia sare ya 1-1 ndani ya dakika 90.

Kwa upande wa Simba, yenyewe ilianza kwa kuitoa Zimamoto kwa mabao 3-1 kabla ya nusu fainali kuitoa Azam FC kwa penalti 3-2 baada ya sare tasa ndani ya dakika 90.

Hivyo, leo timu hizo zitashuka dimbani kila moja ikiwa imejiandaa vema kuweza kupambana na kutwaa ubingwa huo zilioukosa kwa muda mrefu sasa.

Kwa mara ya mwisho Mtibwa kuutwaa ubingwa huo ilikuwa mwaka 2010 ilipotinga fainali dhidi ya Ocean View ya Zanzibar wakati huo kocha wa sasa wa timu hiyo, Zuberi Katwila akiwa mchezaji.

Hivyo, ni dhahiri leo atataka kulibeba kombe hilo ili kuweka rekodi ya kulitwaa na klabu hiyo akiwa mchezaji na hatimaye kocha.

Lakini mchezo wa leo utakumbushia fainali ya mwaka 2015 timu hizo zilipokutana fainali kwenye michuano hii na Simba kuutwaa ubingwa huo kwa ushindi wa penalti 4-3.

Na tangu kipindi hicho, Simba haijawahi tena kulibeba kombe hilo zaidi ya mwaka jana kukaribia kulitwaa, lakini ikajikuta ikilikosa baada ya kufungwa mabao 2-1 na Azam FC katika mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Gombani, Pemba.


Hivyo, tunaamini timu zote zimejiandaa kutoa burudani ya kutosha ili kuwafanya Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla kuhitimisha sherehe za Mapinduzi kwa furaha na amani.

Aidha, tulishuhudia katika michezo iliyopita kukijitokeza changamoto ya waamuzi kushindwa kumudu mchezo, hivyo tunatoa wito kwa waandaaji wa michuano hii kupanga waamuzi bora na watakaotenda haki kwa kufuata sheria 17 za soka.

Na kwa wachezaji watakaoshuka dimbani leo, tunataka kuona wakicheza soka la kiungwana zaidi na kuepuka rafu ambazo zinaweza kusababishiana majeraha yatakayowaweka benchi kwenye mechi zijazo za Ligi Kuu Bara.

Tunatambua baada ya mechi hii ya fainali timu zitarejea kwenye Ligi Kuu, hivyo Nipashe tunatamani kuona wachezaji wakionyesha viwango na burudani zaidi na si vita vya kuumizana. Tunazitakia fainali njema Simba, Mtibwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwanasoka hadharau hata Kombe la Mbuzi

Na Adam Fungamwango

**"HAYA** ni mashindano ambayo tulikuwa makini na wachezaji wetu wasipate majeraha, ili tukirudi kule kwenye ligi tuwe na nguvu zaidi." Ni baadhi ya maneno ya Ofisa Uhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz akizungumza kwenye Uwanja wa Amaan Zanzibar baada ya timu yao kutolewa kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Mtibwa Sugar.

Ameongea maneno mengi, lakini leo naangalia maneno yake haya ambayo amejaribu kuyazungumza, nadhani kuwapoza mashabiki wa Yanga wachukulie kama viongozi hao na benchi lao la ufundi hawakuwa wakiyatolea macho mashindano hayo.

Kuna baadhi ya mashabiki walikwenda mbali sana na kusema kuwa ofisa huyo ameyadharau mashindano hayo ambayo yana heshima kubwa Zanzibar, kwani yanafanyika wakati wa kumbukumbu ya Mapinduzi ya kisiwa hicho kila mwaka.

Kwangu mimi sidhani kama Nugaz ameyadharau la hasha. Ila amefanya hivyo kuwapoza tu baadhi ya wanachama na mashabiki wa Yanga kuonyesha kuwa hawakuwa na mpango na michuano hiyo na akili yao iko kwenye Ligi Kuu Bara.

Simwambii Nugaz, tu, bali wanamichezo wote ambao wana fikra kuwa michuano pekee muhimu ni ligi basi atakuwa anakosea na ninakuwa na wasiwasi na uanamichezo wake.

Michezo ni michezo tu. Ndiyo maana hata uswahilini klabu zinaingia kwenye michuano ya kugombea mbuzi tu, lakini zinakodisha wachezaji mpaka wa Ligi Kuu kwa gharama kubwa.

Pesa anayolipwa mchezaji mmoja wa Ligi Kuu, unaweza kununua hata mbuzi watatu.

Klabu inakodisha wachezaji hata watano mpaka sita wa Ligi Kuu na michuano inaendeshwa wakati mwingine mwezi mzima, timu inayofika fainali na kuchukua mbuzi inaweza kucheza hata mechi sita mpaka nane, inaingia gharama za chakula kwa wachezaji, usafiri na maandalizi mengine ya mechi, lakini inakuja kuambulia mbuzi mmoja tu. Tena utakuta viongozi wa klabu na mashabiki wao wanafurahi na kuweka rusha roho ambalo nalo wanaingia gharama, na kununua mchele kwa ajili ya sherehe za kumtwaa mbuzi. Kwa nini wanafanya hivyo? Kwa nini waingia gharama kubwa kwa sababu ya mbuzi tu? Lengo hapo si mbuzi, ila wana moyo wa uanamichezo.

Mwanamichezo wa ukweli hadharau kombe, au michuano yoyote na wala hawezi kuwaambia wachezaji wasikaze kwa sababu ni michuano midogo.

Kama suala ni majeruhi, ni kwamba mchezaji anaweza kupata kuwa majeruhi hata kwenye mazoezi na si kwenye michuano ya Mapinduzi tu.

Ninavyojua klabu, kocha au mchezaji huwa wanaangaliwa thamani kwa kuchukua mataji na haijalishi ni ligi, FA au michuano mingine mbalimbali, yote inahesabika na kuingia kwenye wasifu.

Ndiyo maana hata Ulaya, timu zinacheza michuano mingi kama Ligi ya Mabingwa, Europa, ligi ya ndani, Komba la FA na mengine kama Ngao ya Jamii ambayo makocha na wachezaji huchukulia kwa uzito ule ule na pia huyaheshimu na kuyahesabu wanapoyatia kwenye makabati yao.

Hapa kwetu tu ndiyo kuna baadhi ya watu ambao wao wanachoonekana kuheshimu ni Ligi Kuu tu, kwa sababu eti ndilo linaloa mwakilishi wa kwenda kushiriki katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ikumbukwe kuwa bingwa wa ligi ni mmoja tu, klabu au kiongozi anayeonekana anadharau michuano mingine, akikosa ubingwa ina maana kaisababisha timu yake ikose taji lolote kwa msimu huo.

Yanga ilianzishwa mwaka 1935 na Simba 1936, Ligi Kuu ilianzishwa mwaka 1965, hii ina maana kuwa klabu hizo kabla ya ligi ilikuwa ikicheza michuano au vikombe vingine mbalimbali nchini.

Hapa ndipo inapoonyesha kuwa viongozi wa klabu hizi zamani na zingine zilizokuwapo walikuwa ni wanamichezo wa kweli kwa sababu hawakudharau michuano hiyo na hata Ligi Kuu ilipoanzishwa bado kulikuwa na vikombe vingi kama Kombe la Hedex, Kombe la CCM, Kombe la Nyerere, Kombe la Jengo, Kombe la Ofuma na mengine mengi, kila timu ikija na kikosi kamili wakati mwingine Simba na Yanga zikikutana fainali.

Hii ya kudharau michuano siku hizi na kusema kuwa wachezaji wataumia inatoka wapi?

## MJADALA

## Mitihani ituibulie vipaji

**Mhariri,**

*SISI tuliosoma katika zama hizo, kwetu msimiati unaoitwa mitihani ni kazi kubwa kuliko hata namna tunavyoutafakari.*

*Neno mtihani kwetu lilikuwa zito sana na ilikuwapo ya hatua nyingi; darasa la nne, nane, sekondari, kidato cha nne, sita na kadhalika.*

*Unapofika kipindi cha mwanafunzi kujisomea akijiandaa kwa mitihani, ufanyaji wake na pazito zaidi ni matokeo kama ya juzi, huwa msukosuko wa 'kukata na shoka' katika mtazamo wa ama kupata au kukosa.*

*Najua mwisho wa wiki iliyopita ulikuwa na yote hayo, kicheko na kununa kwa kila namna ilivyo kawaida ya yote. Inafanana sana na matokeo ya michezo kama vile soka, kikapu na ngumi inapokuwa na hamasa kwa umma unaoizunguka.*

*Binafsi, nakumbuka huko nyuma kuna wakati tulipata simulizi za aliyekuwa Dikteta Adolph Hitler, ambaye alisema maishani mwake alihofu jambo moja tu la mtihani.*


*Kwa mamlaka za kiserikali, ni wakati sahihi zaidi kwao unapofika wakati huu kufunguka kuwafuatilia vijana mmoja mmoja waliofanya vizuri katika mitihani yao, nje ya mfumo rasmi kama ya watoto wenye vipaji.*

*Ni kwa namna hii ndiko Watanzania wenye makuu yao kitaaluma, manufaa yao yanaurudia umma katika namna mbalimbali na Taifa linajengeka, kupitia nyenzo ya vipaji.*

*Nakumbuka huko nyuma, Waziri Mkuu ambaye sasa ni mstaafu, Mizengo Pinda, alihimiza mtazamo unaofanana na huo, kuhusu uendelezaji vijana wenye vipaji, kwa manufaa ya taifa katika siku zijazo.*

**Mwalimu mstaafu,**
**S. S Mahrusu,**

# Sakata la Nchimbi liwe funzo wachezaji wa mkopo




**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE straika Ditram Nchimbi alicheza mechi yake ya kwanza akiwa na Yanga siku ya Januari 4, mwaka huu, timu yake ilipocheza na mahasimu wao wa jadi Simba kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na kutoka sare ya mabao 2-2.

Ina maana sakata lake la usajili limemalizika baada ya kuchukua nafasi kubwa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa wiki kadhaa.

Nchimbi, aliyekuwa akiichezea Polisi Tanzania kwa mkopo kutoka Azam FC, alikuwa akihitajiwa kwa udi na uvumba na Yanga, hasa baada ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi kati ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga na Polisi Tanzania, zikatoka sare ya mabao 3-3.

Yanga iliona ni straika anayefaa kuwa kwao, na ikapiga hodi Azam FC kumtaka, nao hawakuwa na hiyana, kwa sababu ni mchezaji wao, ikamuuza.

Kitendo hicho kiliwakasirisha viongozi wa Polisi Tanzania na kupinga usajili huo kwa madai kuwa hawakushirikishwa.

Wakasema kuwa wao walimchukua kwa mkopo wa mwaka mmoja, lakini wanashangaa kuona baada ya nusu mwaka tu, tayari Azam wanamtaka mchezaji wao na wanawauzia Yanga wakati wao ndiyo waliompandisha kiwango na thamani kiasi cha kuitwa mpaka kwenye timu ya Taifa Stars.

Pamoja na maneno yote hayo, lakini ukweli ukabaki pale pale kuwa Azam na Polisi Tanzania walipeana mchezaji hiyo kwa maneno zaidi bila maandishi.

Kwa maana hiyo kesi hiyo ikawa rahisi kwa Azam kushinda, wakamchukua mchezaji wao na kuwauzia Yanga, Polisi Tanzania wakabaki wanashangaa.

Ukiangalia sakata zima utagundua kuwa soka letu Tanzania bado lina matatizo na lina sehemu nyingi za kurekebishwa, hadi kwenye taratibu na kanuni.

Bado baadhi ya viongozi wa soka wanachukulia kama wachezaji wa mkopo ni wale tu ambao wamekwisha, au hawapati nafasi kwenye timu moja, hivyo kupelekwa kwenye timu nyingine kwa ajili ya kupunguza idadi ya wachezaji.

Na hata klabu zinazopokea wachezaji hao ziwachukua tu kana kwamba zinasaidiwa tu, hivyo wanawachukua kwa mali kauli bila maandishi.

Kama sakata la Nchimbi lingewekwa kwenye maandishi sidhani kama kungekuwa na mtafaruku wowote ule.

Kama Azam ilikubali kumtoa kwa mkopo na Polisi Tanzania kukubali kumpokea, zingekaa na kuandikishiana mkataba wa mkopo wenye vipengele ambavyo vingewasaidia kwenye mwongozo kama tatizo lolote likitokea.

Nadhani mwanzoni kila klabu ilichukulia poa kwa sababu wachezaji wengi wa mkopo bongo ni aghalabu sana kwenda kufanya vizuri anakokwenda, lakini ikawa kinyume kwa Nchimbi.

Tunashukuru kuwa limemalizika, lakini sakata hilo liwe funzo kubwa kwa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Bodi ya Ligi na klabu zote za Tanzania.

TFF na Bodi ya ligi sasa iweke sharti la wachezaji wote wanaotoka na kwenda kwa mikopo kwenye klabu zingine, wawe na mikataba ya mikopo yenye vipengele muhimu.

Hii itawasaidia kufanya uamuzi kama tatizo likijitokeza kwa kutumia vipengele vile vile vya mikataba walioandikishana.

Klabu ziandikishiane muda kamili wa mkopo, lakini ukiwa na kipengele kuwa hatorudishwa au kuuzwa kwa muda wote labda wa mwaka mmoja akiwa na timu aliyopelekwa kwa mkopo.

Vipengele kama hivi au vinavyofanana na hivi ni muhimu ili likitokea la kutokea kama lilivyotokea kwa Nchimbi, wala hatu hawaumizi kichwa.

Kuna vipengele vingine kama nani atakayelipa mishahara, au klabu zote zitalipa nusu kwa nusu, pia kuna klabu zinawekeana kuwa mchezaji huyo hatocheza kwenye mechi ambayo timu iliyopewa mchezaji wa mkopo itapambana na timu yake mama.

Hivi ni vipengele muhimu ambavyo vinawekwa sana kwa wenzetu, lakini kwenye soka la Bongo wanalichukulia poa nadhani kwa sababu halijawahi kutokea kama hili la Nchimbi.

Ndiyo maana nasisitiza kuwa suala hili liwe somo kwa mamlaka za soka, klabu za Tanzania na wachezaji wenyewe.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed




## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Usafiri wa reli warejea baada ya miezi mitatu

**Na Dege Masoli,**
MUHEZA

USAFIRI wa njia ya reli umerejea tena, baada ya huduma hiyo kusimama kwa takriban miezi mitatu kutokana na daraja kusombwa na maji wilayani Muheza mkoani Tanga.

Meneja wa Reli Kanda ya Kaskazini, Ramadhani Gombo, aliwaambia waandishi wa habari kuwa usafiri huo umerejea baada ya kukamilika kwa matengenezo makubwa ya daraja hilo wilayani hapa na maeneo mengine ya njia hiyo.

Gombo alisema huduma ya usafirishaji wa mizigo kati ya Tanga na mikoa ya Kanda ya Kaskazini ulisimama kwa kuwa licha ya kusombwa na maji kwa daraja hilo, lakini baadhi ya maeneo ya njia hiyo yaliharibiwa vibaya na mvua hizo.

Alieleza kuwa tangu mwishoni mwa mwaka jana sambamba na daraja hilo mvua hizo ziliharibu maeneo mbalimbali ya njia hiyo na kuifanya ishindwe kutumika na hivyo usafirishaji wa mizigo kusimama kwa muda huo. Alisema athari za mvua hiyo zilianza Oktoba 10, mwaka jana, ambapo Shirika la Reli Tanzania (TRC)lililazimika kuanza kuyafanyia ukarabati maeneo hayo Novemba kwa kurekebisha na kuondoa maji eneo lenye daraja hiyo na kuanza kazi hiyo.

"Mbali ya daraja hilo kusombwa na maji lakini mvua hiyo iliathiri maeneo mengine kama vile Korogwe, Mnyuzi na Gendagenda ambayo kwa kutopitika kwake ilitilazimu nayo kuyafanyiakazi na sasa mambo ni mazuri," alisema Gombo.

Alieleza kuwa ukarabati huo ulikamilika Novemba 23, mwaka jana ambapo mapema Januari mwaka huu baada ya kukamilisha daraja la Muheza huduma hiyo ilianza kurejeshwa na sasa wafanyabiashara wameanza kupitisha mizigo yao kama kawaida.

Akifafanua kuwa hasara iliyotokana na kusimama kwa huduma hiyo kuwa ni kukosa shehena za mizigo hususani inayotoka Bohari ya Mafuta mkoani Tanga (GBP) na ya saruji waliyokuwa wakiisafirisha kwenda mikoa ya Kilimanjaro, Dar es Salaam na mikoa mingine Kanda ya Ziwa.



Muuza vinyago na picha za kuchora katika Manispaa ya Moshi, James Mallya maarufu Ras Jimmy (kulia), akimuuzia mteja wake anayejishughulisha na shughuli za utalii, Kushi Timbuktu, picha ya kuchora kwa ajili ya kuwauzia watalii katika eneo la jengo la Fresh Business Centre mjini Moshi jana. **PICHA: JAMES LANKA**

# Shein adokeza ongezeko mishahara

**INATOKA UK. 2**

kipindi cha miaka tisa ya utawala wake katika sekta ya afya, elimu, uchumi na miundombinu.

"Kasi ya ukuaji uchumi iliongezeka kutoka asilimia 4.3 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 7.1 mwaka 2018, pato la taifa limeongezeka kutoka Sh. bilioni 1,768 mwaka 2010 hadi kufikia Sh. bilioni 2,874 mwaka 2018," alisema Rais Shein.

Alisema lingine ni Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar, Dira ya Maendeleo ya mwaka 2020 pamoja na Maendeleo ya Kimataifa.

**KUKUA KWA PATO**

Rais Shein alisema vilevile, pato la mwananchi nalo limeongezeka kutoka wastani wa Sh. 942,000 sawa na Dola za Marekani 675 mwaka 2010 hadi Sh. milioni 2,323,000 sawa na Dola za Marekani 126,000 mwaka 2018.

**MFUMUKO WA BEI**

Alisema mfumuko wa bei nao umepungua kutoka asilimia 14.7 mwaka 2011 hadi kufikia asilimia 3.9 mwaka 2018, utekelezaji wa miradi ya maendeleo 304 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 3.42 iliyotengeneza ajira 16,866 hadi mwaka 2018.

**SEKTA ELIMU**

"Kwenye sekta ya elimu tumefanikiwa kuainisha elimu bure, shule zimeongezeka, idadi ya wanafunzi imeongezeka, hadi mwaka 2019 shule za awali zilikuwa 382 zikiwa na wanafunzi 85,984 ikilinganishwa na mwaka 2010 kulikuwa na shule 238 na wanafunzi 29,782," alisema Rais Shein.

Alisema shule za msingi zimeongezeka kwamba mwaka 2010 kulikuwa na shule 299 zikiwa na idadi ya wanafunzi 226,812, mwaka 2019 zimeongezeka na kufikia shule 381 zikiwa na wanafunzi 290,510. Alisema shule za sekondari nazo zimeongezeka, kwamba mwaka 2010 kulikuwa na shule 105 zikiwa na idadi ya wanafunzi 80,208, mwaka 2019 zimefikia shule 284 zikiwa na idadi ya wanafunzi 130,713.

Rais Shein alisema bajeti ya sekta ya afya imeongezeka kutoka Sh. bilioni 10.81 mwaka 2010/11 na kufikia Sh. bilioni 104.24 mwaka 2019/20.

"Idadi ya kusomesha madaktari imeongezeka, kwa sasa daktari mmoja anatibu wagonjwa 6,276 kulinganisha na mwaka 2010 kwamba daktari mmoja alikuwa anatibu wagonjwa 31,838," alisema Rais Shein.

Alisema serikali ya Zanzibar imejitahidi katika kuongeza mishahara ya watumishi wa umma tangu maka 2010, hali iliyotokana na makusanyo mazuri ya mapato.

Alisema serikali ya Zanzibar imeongeza malipo ya wastaafu kwa mwezi kutoka Sh. 25,000 mwaka 2017 hadi kufikia Sh. 90,000 mwaka 2019.

**Imeandaliwa na Rahma Suleiman (Zanzibar) na Gwamaka Alipipi, Dar**

## Watumishi ardhi wabanwa kujieleza

**INATOKA UK. 3**

wote wa ardhi, bali unasaidia kuwafuatilia wamiliki wanaokwepa kilipa kodi ya ardhi jambo alilolieleza lisiposimamiwa kwa umakini litapunguza wigo wa ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

"Uingizaji viwanja kwenye mfumo wa kielektroniki ulianza tangu mwaka 2017, lakini bado hakuna kilichofanyika hatuwezi kulea uozo huu unaoweza kuwapa mzigo wateja kutokana na malimbikizo ya kodi," alisema Mabula.

Mabula alisema wizara yake inataka kuwa na malengo yanayoendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano na kuiagiza Ofisi ya Ardhi ya Kanda kupitia takwimu za viwanja vilivyo katika mfumo kwa halmashauri za mkoa wa Mbeya na kusisitiza haiwezekani kuwa na Ofisa Ardhi Mteule ama Mkuu wa Idara ya Ardhi asiyefuatilia na kusisitiza katika suala hilo wizara yake haitakuwa na msamaha.

Kuhusu ukusanyaji wa kodi ya ardhi, waziri huyo alionyesha kutoridhishwa na makusanyo ya kodi hiyo kwa halmashauri za mkoa wa Njombe na kwamba kufikia Desemba 2019 halmashauri zote zilikusanya jumla ya Sh. 369,863,643.34.

Alisema kiasi hicho kiko chini ya asilimia 50 ya makusanyo ya kodi ya ardhi katika mkoa huo uliokuwa na lengo la kukusanya Sh. bilioni 1.2.

Katika hatua nyingine, waziri huyo alikagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa kwa gharama ya takriban Sh. bilioni 2.7.

Mabula mbali na kuridhishwa na ujenzi wa jengo hilo amelitaka NHC kuhakikisha jengo hilo linakamilika mapema iwezekanavyo kwa kuwa lilichelewa kukamilika kutokana na changamoto mbalimbali.

## Marufuku ujenzi bila kibali

**INATOKA UK. 2**

jijini Dodoma uliodumu kwa takribani miaka 14.

Aidha, ametoa miezi mitatu kwa Halmashauri ya Jiji, Idara ya Ardhi Mipango Miji na Rasilimali Watu kuhakikisha wanakamilisha upimaji na urasimishaji katika eneo hilo.

Alisema mgogoro huo umedumu kwa muda mrefu na kwamba serikali imeamua kuumaliza kwa kurasimisha wananchi waliojenga kiholela na kupima maeneo yote ambayo hayajapimwa.

Aidha, Waziri Lukuvi baada ya kusikiliza wananchi na kupitia hati zao ilibainika kuwa asilimia kubwa ya hati zimemaliza muda wake wa miaka 33 tangu zitolewe mwaka 1985, na kusisitiza kuwa kwa sasa ardhi hiyo siyo mali yao bali ni mali ya Rais hivyo irejeshwe kwake kwa matumizi yanayotolewa mwongozo upya.

**ONYO KWA WANANCHI WAKOROFI**

Aliwaonya wananchi wa eneo hilo wenye tabia ya kutumia silaha kama mapanga na mishale na kuzuia watumishi wa serikali kufanya kazi yao kuacha tabia hiyo mara moja.

"Ninyi mnaojifanya mnajua kutumia silaha za upinde, mishale, sime na mapanga, muache tabia hiyo mara moja, maana serikali ina silaha za moto... sasa ole wenu muwazuie watendaji wa Jiji kufanya kazi yao ya upimaji na kuchelewesha kazi hiyo, tutawashughulikia ba'rabara," alisema Lukuvi.

Alisema baada ya wananchi hao kupimiwa, watalipa gharama za kodi ya serikali zitakazokuwa zimepangwa na kuruhusiwa kuanza ujenzi au kuendelea na ujenzi.

HABARI KITAIFA

# Simbachawene akifungia kiwanda cha nondo

**Na Mwandishi Wetu,**
MKURANGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, amekifunga kiwanda cha kuzalisha nondo cha Fujian Hexingwang kilichopo Kisemvule wilayani Mkuranga katika Mkoa wa Pwani, kwa ukiukwaji mkubwa wa sheria na kanuni za mazingira.

Akizungumza baada ya ziara ya kushtukiza mwishoni mwa wiki katika kiwanda hicho mbali ya kukifungia kiwanda hicho, ameutaka uongozi wa kiwanda kutatua kero za wananchi ili kiweze kurejea na kuendelea na uzalishaji.

"Naiagiza NEMC kufuatilia taratibu zote ili kuhakikisha kiwanda hakiendelei kuwa katika mazingira ambayo nimeyakuta hapa baada ya mwezi mmoja kupita, tunavita sana viwanda lakini ustawi wa watu wetu na mazingira ni jambo muhimu sana," alisema Simbachawene.

Simbachawene aliongeza kuwa kiwanda hicho kitatozwa faini kwa kukiuka sheria na kanuni za mazingira zinazowataka wamiliki wa viwanda kufuata taratibu zote kabla hakijaanza uzalishaji.

"Kuna mambo ya ajabu nimeyakuta katika kiwanda hiki, wanaendelea na uzalishaji huku wakiwa hawajakamilisha ujenzi wa miundombinu jambo ambalo ni kinyume na sheria na kanuni zetu hapa nchini, hivyo kitatozwa faini kwa ukiukwaji huo wa sheria na kanuni," alisisitiza Simbachawene.

Kwa upande wao wakazi wa eneo linalozunguka kiwanda, walisifu maamuzi yaliyotolewa na Waziri kwani kwa muda mrefu sasa wamekuwa waathirika wa kero zinazotokana na kiwanda hicho.

"Maamuzi haya ya serikali yanatupa ahueni kubwa sisi wakazi wa eneo hili la Kisemvule kwani kiwanda hiki sio rafiki kwa maisha yetu. Tumekuwa tukiathirika na kelele za usiku na mchana, vumbi na harufu kali hali inayochangia uwepo wa magonjwa kwa wakazi wa eneo hili," alisema Shaban Athumani.

Naye Daniel Saul, alisema hawapingi azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda kwa kuwa vinachochea ukuaji wa uchumi badala yake ameitaka serikali kuwa na viwanda ambavyo vitakuwa rafiki kwa ustawi wa watu na mali zao.

"Tunaishukuru sana serikali kwa jitihada zake za kuimarisha uchumi kupitia viwanda, tunafarijika kama wananchi lakini vile ambavyo vinakiuka taratabu, kanuni na sheria za mazingira vichukuliwe hatua kwa faida ya ustawi wa kizazi cha leo na kesho,'" alisema.

Kaimu Meneja wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Mashariki, Ndimbumi Joram amesema NEMC hawatakuwa na muda wa kupoteza katika kuteleleza maagizo ya waziri kwa kuwa ni jukumu lao kuhakikisha mazingira yanalindwa kwa faida ya watu wote.

"Wote tumesikia maagizo ya Waziri na NEMC tunaanza kuyafanyia kazi mara moja kwa kuuandikia uongozi wa kiwanda hiki barua rasmi na tutawafuatilia kwa ukaribu kwa kipindi chote walichopewa ili wafanye marekebisho ya miundombinu," alisema na kuongeza kuwa wenye viwanda lazima wafuate taratibu, kanuni na sheria kabla hawajaanza uzalishaji.




Ofisa Mifugo Kata ya Bulige, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, Dk. David Sospiter, akimchoma punda sindano ya kumkinga na magonjwa ya ngozi na minyoo katika viwanja vya Shule ya Msingi Segese kwa ufadhili wa Shirika lisilo la Kiserikali la Kutetea Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO). **PICHA: SHABAN NJIA**

# Bangi yampeleka jela miaka mitatu

**Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imemuhukumu mkazi wa Wilaya ya Rufiji, mkoani Pwani, Karimu Abdallah Dadi (22), kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. 1,800,000 baada ya kukutwa na hatia ya kumiliki dawa za kulevya aina ya bangi yenye uzito wa kilo 14.13.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Muyonga Magala, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Hakimu Magala alimuuliza mshtakiwa iwapo ana lolote la kuiambia mahakama isimpe adhabu kali, kufuatia shtaka linalomkabili.

Baada ya kupewa nafasi hiyo alijitetea kwa kuiomba mahakama isimpe kwani ni mkosaji wa mara ya kwanza. Pia alidai anayo familia inayomtegemea akiwamo mke na mtoto, hivyo iwapo atapewa adhabu kali kutawafanya wakose huduma zake, na kwamba alilazimika kushiriki biashara hiyo ikiwa ni sehemu ya kujitafutia riziki isaidie na familia yake. Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, aliiomba Mahakama impatie mshtakiwa adhabu kali, kwani vitendo vya utumiaji wa dawa za kulevya ni uhalibu.

Akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 43/2019 kupitia kifungu cha Sheria namba 15 A (1) na 2 (c) Act namba 5/2015 kilichofanyiwa marejeo namba 15/2002, Hakimu Magala alimuhukumu kifungo cha miaka mitatu gerezani au kulipa faini ya Sh. milioni 1.8.

Hata hivyo, mshtakiwa alishindwa kulipa faini, hivyo kulazimika kwenda gerezani kutumikia adhabu.

Awali, ilidaiwa na Mramba kuwa mshtakiwa alikamatwa Machi 22, mwaka jana majira ya asubuhi eneo la Chuo cha Ufundi (VETA) na askari Polisi waliokuwapo eneo hilo, akiwa anasafiri na kusafirisha bangi hiyo yenye uzito wa kilo 14.13 ndani ya basi la Kampuni ya Swahili Travel T 569 DFA, kutoka Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara kwenda Rufiji mkoani Pwani.

## Ushirika michikichi walia mkopo TADB

**Na Ashton Balaigwa,**
KIGOMA

MUUNGANO wa Vyama 13 vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) mkoani Kigoma vilivyoitikia agizo la serikali la kulima kilimo cha zao la michikichi wamemwomba Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwasaidia kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha ili kuendesha kilimo hicho.

Ombi hilo limekuja baada ya AMCOS hiyo kushindwa kupata mkopo mpaka sasa kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), licha ya kutimiza baadhi ya masharti ikiwamo kufungua akaunti pamoja na kuweka fedha.

Mwenyekiti wa Wenyeviti wa AMMCOS, Husein Ally, alisema baada ya kuitikia wito huo changamoto iliyopo hivi sasa ni upatikanaji wa mbegu za michikichi aina ya tenera pamoja na fedha kwa ajili ya kufanya shughuli ya kuendesha kilimo hicho kwa kuwa kinahitaji gharama kwa ajili ya matunzo.

Alisema alipofanya ziara katika Mkoa wa Kigoma mwaka jana kwa ajili ya kuhamasisha kilimo cha michikichi alizitaka AMCOS hizo kuungana na kulima cha zao hilo na kuagiza benki hiyo kuwapatia mkopo kuendesha kilimo hicho, lakini mpaka sasa hawajapata.

"Moja ya masharti tuliombiwa na benki hiyo ni pamoja na kufungua akaunti na kuweka fedha kama dhamana na tulichanga na kuweka asilimia 10 ya mkopo, lakini mpaka sasa tumefuatilia tunazungushwa tu," alisema mwenyekiti huyo.

Akijibu kuhusu changamoto ya ukosefu wa mbegu, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) Dk. Geoffrey Mkamilo, alipongeza AMCOS hiyo kwa kuitikia agizo la Waziri Mkuu, na kwamba wakulima kutoka katika muungano wa vyama hivyo watapatiwa bure miche ya michikichi aina ya tenera kwa kuwa miche hiyo imezalishwa ya kutosha.

# Sababu walimu kufundishwa Tehama

**Na Enock Charles**

SERIKALI imekusudia kuwajengea uwezo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) walimu wanaofundisha shule za msingi na sekondari ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani.

Lengo lingine la mpango huo ni kurahisisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa kazi zao za ufundishaji katika jitihada za kufikia malengo ya Tanzania ya Viwanda.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa utolewaji wa mafunzo kwa wakufunzi wa vyuo vya ualimu nchini, Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Sebastian Inoshi, alisema mafunzo hayo yatawajengea uwezo wa kiteknolojia katika habari na mawasiliano ili waweze kuwafundisha walimu katika vyuo.

"Mafunzo haya yaliyochukua takribani siku kumi ni kwa lengo la kuwajengea wakufunzi wetu katika vyuo vyote 35 vya ualimu nchini ili na wao wakawafundishe wanafunzi wao ambao ni walimu wa shule za msingi na sekondari katika masuala ya Tehama," alisema Inoshi.

Mafunzo kama hayo yameshatolewa katika kanda nne kati ya sita, na sasa yanaendelea katika Kanda ya Ziwa Magharibi inayojumuisha vyuo vya ualimu Bunda, Mulutunguru, Katoke, Butimba, Tarime, Ndala, Kabanga, Shinyanga, Tabora na Kasulu kwa jumla ya wakufunzi 269 yanayotolewa katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kwa upande wa Kanda ya Kaskazini, mafunzo hayo yanatolewa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya Chuo hicho ikijumuisha vyuo vya ualimu Mandaka, Korogwe, Mamire , Marangu, Monduli, Patandi, Singachini na vyuo vingine ambavyo havikupata mafunzo hayo kwa awamu ya kwanza kwa jumla ya wakufunzi 205.

Mmoja ya wanufaika wa mafunzo hayo, Wakuru Manini kutoka Chuo cha Ualimu Patandi, alisema ni ya muhimu ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto za mawasiliano na kuwaongezea kasi na ufanisi katika majukumu yao katika ulimwengu wa sasa ulio na maendeleo makubwa katika teknolojia ya habari na mawasiliano.

"Mafunzo haya ni ya muhimu kuendeleza ujuzi kwa walimu kwa sababu teknolojia kwa sasa ndio suala la msingi litakalomwezesha mwalimu katika kukabiliana na changamoto za kimawasiliano na kumwandaa mwanafunzi kwa ufanisi," alisema Inoshi.

Naye Mkufunzi Richard Nguma kutoka Chuo cha Kabanga, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Canada kwa kuanzisha mpango wa mafunzo ya Tehama kwa wakufunzi wa vyuo vya ualimu nchini kwa kuwa yatawasaidia walimu kufanya maandalizi bora ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

# Gulio bidhaa zilizotumika Dar kuanza Machi

**Na Elizabeth Zaya**

GULIO la kuuza bidhaa zilizotumika limeanzishwa jijini Dar es Salaam huku wananchi wakiombwa kuchangamkia fursa hiyo kuuza bidhaa ambazo hawazitumii.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Kampuni ya Masoko ya Gateway Buy and Sell, Reherma Moses, gulio hilo litakuwa linatumika kuuza bidhaa zilizotumika kila baada ya miezi mitatu na kwamba linatarajiwa kufanyika mwanzoni mwa Machi mwaka huu katika viwanja vya Tanganyika Parkers, Kawe. Alitaja baadhi ya bidhaa zitakazokuwa zinauzwa katika gulio hilo kuwa ni pamoja na nguo, viatu, mashuka na vitu vya ndani vilivyotumika.

Kwa mujibu wa Moses, gulio hilo limeanza na litafanyika kwa mara nyingine Machi mwaka huu na kuwataka wajasiriamali kujitokeza kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema dhumuni la gulio hilo limelenga kuwasaidia wananchi kuuza bidhaa walizozichoka ambazo zimekuwa mzigo katika nyumba zao.

"Wapo watu ambao nyumbani kwao kuna bidhaa ambazo hawazitumii lakini bado zinafaa kutumika na watu wengine, hivyo badala ya kuziacha kuendelea kuwapo ndani ya nyumba tukaamua kuanzisha gulio ambalo litasaidia na wengine kufaidika hata kama wana kipato kidogo," alisema Moses.

"Kwa mfano wapo kinamama ambao wamenunua begi nyingi za mkononi na hawazitumii, gulio hili litafanya kazi hiyo, badala ya kuziacha ziharibike ndani, watauza kwa wengine na bidhaa nyingine zinazofanana na hizo."

"Tumeamua kuanzisha gulio hili baada ya kufanya uchunguzi na kubaini kwamba kuna bidhaa ambazo zinaharibika kutokana na watu kutozitumia, wakati bado zinahitajika kuwasaidia wengine."

Mmoja kati ya waliojitokeza kwenye gulio la kwanza kuuza bidhaa zao, Farssy Kassim, alipongeza kuanzishwa kwake na kwamba amelitumia kuuza bidhaa mbalimbali ambazo alikuwa hazitumii.

"Magulio kama haya yamekuwa yakifanyika zaidi nchi za Ulaya na Amerika na yana faida kubwa kwa maana hakuna bidhaa zinazotupwa, pia inawasaidia wale wasio na kitu kupata kitu kwa gharama ndogo tena zina ubora."



Spika mstaafu wa Bunge, Anna Makinda, ambaye ni Mama Vifurushi katika Sekta ya Bima ya Afya ya Serikali, akimkabidhi kadi ya matibabu ya bima ya afya (NHIF)mmoja wa wananchi waliojiunga na huduma hiyo, katika uzinduzi wa vifurushi vya Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya jijini Mwanza juzi. **PICHA: ROSE JACOB**

# Wakazi kisiwani wapata majisafi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANANCHI wa Kisiwa cha Kokota Wilaya ya Wete wametakiwa kutunza vyanzo vya maji pamoja na kulipa ada ya huduma hiyo kwa wakati ili mamlaka husika iweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi zaidi.

Hayo yalielezwa na Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, Said Soud Said, alipokuwa akizungumza na wananchi wa kisiwa hicho kwenye ufunguzi wa mradi wa majisafi na salama katika kijiji cha Mkanjuni Mtambwe.

Soud alisema kuwa anatambua kuwa miundombinu ya maji inatumia gharama kuwa katika kuianzisha na kuiendeleza, hivyo wananchi hawana budi kuitunza kwa maslahi mapana kwa taifa.

"Niishauri Mamlaka ya Maji ijitahidi kushirikiana na wananchi katika kuutunza mradi huu ili uweze kuleta manufaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo," alifahamisha Said.

"Nimpongeze Salama Aboud Talib, Waziri wa wizara hii kwa kuwa makini na kusimamia sekta ya maji kwa kuhakikisha upatikanaji na usimamiaji wa huduma hii kwa wananchi wote," alisema Said.

Soud alisema aliwataka wananchi hao kutumia huduma hiyo kwa misingi na kanuni za afya bora ili kujiepusha maradhi yanayohusiana na huduma ya majisafi na salama na watajenga taifa imara lenye watu wenye afya nzuri.

Aiipongeza Taasisi ya Millelle Foundation kwa juhudi zake za kushirikiana na serikali katika kuwatatulia wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba matatizo yao.

"Millelle Foundation ni mfano wa kuigwa hapa Zanzibar kwani imekuwa ikijitolea kwa hali zote katika kusaidia maendeleo ndani ya taifa letu," alisema Soud.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Omar Khamis Othman, alieleza kuwa kwa sasa tatizo la huduma ya majisafi na salama katika kisiwa cha Kokota itakuwa ni histori kwani serikali imefanya jitihada zake zote kuhakikisha wananchi wa kisiwa hicho nao wanafaidika na huduma hiyo.



## HABARI ARUSHA

# Mianzini - Ngaramtoni kunufaika barabara ya lami

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BARABARA inayotoka Mianzini hadi Ngaramtoni,itaanza kutengenezwa Januari 15 mwaka huu ili kutimiza agizo la Rais John Magufuli alilolitoa Desemba 2, mwaka 2018 kuwa itajengwa kiwango cha lami.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa barabara nne jijini hapa, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alisema barabara hiyo ina changamoto na kusababisha usumbufu kwa wananchi, hivyo ukarabati unatakiwa kuanza katika sehemu korofi zote ili kazi ya uwekaji lami iendelee kufanyika bila kikwazo.

Gambo alisema Rais Magufuli alitoa agizo hilo wakati akiweka jiwe la msingi, ambapo alisema hakutakuwapo na ulipaji wa fidia katika sehemu zitakazoguswa na barabara.

"Wananchi walikubali ili waondokane na changamoto wanazopata, hivyo sitaraji kupata changamoto yoyote kwa mwananchi zaidi ya kushirikiana na wajenzi ili barabara yao ikamilike haraka.

"Hakuna mwananchi atakayelipwa fidia yoyote, hivyo mwendelee kushirikiana na serikali kuleta maendeleo ya nchi, barabara ni kitu cha muhimu sana katika shughuli zetu za kiuchumi, sehemu ikiwa na barabara nzuri lazima biashara zishamiri," alisema Gambo. Gambo alipongeza Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) kwa maandalizi ya matengenezo ya barabara hiyo pamoja na kukamilisha vipimo vyote vinavyostahili.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisema wametenga Sh. milioni 157 kwa ajili ya kuboresha maeneo korofi yenye changamoto, wakati wakisubiri kazi kubwa kufanyika ili kusaidia kupunguza foleni. Aidha, Muro alimshukuru Gambo, kwa kufanya ziara hiyo na kuongea na baadhi ya wananchi juu ya ujenzi huo wa barabara.

"Lakini jambo kubwa alilofanya mkuu wetu wa Mkoa kuwakumbusha wananchi juu ya kutolipwa fidia ambayo walishaelezwa na Rais na walikubali mbele yake," alisema.

Naye Meneja wa Tanroads Mkoa wa Arusha, John Kalupale, alisema mradi huo una thamani ya Sh. milioni 580 itakayotumika kwenya barabara yenye urefu wa kilomita 18 na kazi ya usanifu ilishamalizika Desemba mwaka jana.

"Kuanzia Januari 15 tunaanza kazi rasmi ya kutengeneza barabara hiyo, na kuweka kiwango cha lami kama Rais alivyotoa agizo kwenye barabara hiyo," alisema.



Meneja wa Kiwanda cha TBL cha Arusha, Joseph Mwaikasu, akitoa maelezo kuhusiana na mchakato wa uzalishaji wa bia kutumia teknolojia za kisasa kwa wanajeshi kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), walipotembelea kiwanda hicho, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni kwa kusababisha kifo cha muuguzi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

JESHI la Polisi mkoani Manyara, linamshikilia Ofisa Masoko wa Kiwanda cha Bia (TBL), Tumain Baha (30), Mkazi wa Mrara Juu Halmashauri ya Mji wa Babati kwa tuhuma za kugonga na kumsababishia kifo muuguzi wa Hospitali ya Mrara.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Paul Kasabago, alimtaja muuguzi aliyeuawa katika ajali barabarani kuwa ni Christopher Migire (48), mkazi wa Mtaa wa Kwere. Alisema tukio hilo lilitokea Januari 9, mwaka huu majira ya usiku maeneo ya Hospitali ya Mji wa Babati Mrara.

Kasabago alisema gari lililomgonga muuguzi huyo lilikuwa na namba za usajili T. 695 DMW aina ya Toyota Hilux, ambalo lilikuwa likiendeshwa na dereva huyo wa TBL (Tumaini).

Aidha, alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva kushindwa kuchukua tahadhari ya alama za barabarani na kumgonga mtembea kwa miguu, aliyekuwa akivuka barabara kwenye kivuko cha watembea kwa miguu.

"Hapa palikuwa na matuta na kivuko cha waenda kwa miguu, lakini dereva hakujali aliendesha mwendo aliotaka na kusababisha kifo hiki kwa mtembea kwa miguu," alisema.

Alisema mtuhumiwa yupo mahabusu, na kuwa uchunguzi ukishakamilika atapelekwa mahakamani.

Mkazi wa Maisaka, Lilian Laurent, alisema inapofika usiku wapo madereva wanaojisahau na kuendesha kwa kasi, bila kufuata sheria wakijua hamna mtu wa kuwachukulia hatua kwa kuwa askari hawapo barabarani usiku.

# Gambo aiagiza Tanroads kutatua kero Loliondo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameuagiza Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Arusha kufanya ukarabati wa maeneo yasiyopitika kipindi cha mvua, hususani katika mito, mabonde makubwa na makorongo yaliopo kwenye barabara ya Mto wa Mbu - Loliondo.

Gambo alisema lengo ni kuwaondolea wananchi adha wakati wakisubiri ufumbuzi wa kudumu.

Gambo alisema hayo juzi wakati wakati akikagua ujenzi wa barabara hiyo, katika maeneo tofauti, ambapo amejionea maeneo korofi na kutoa maelekezo kwa Tanroads na makandarasi kutafuta suluhu ya maeneo hayo.

"Maeneo haya hayapitiki kipindi hiki cha mvua na kusababisha wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro kukwama katika shughuli zao za kiuchumi, hivyo naagiza Tanroads na makandarasi tafuteni suluhisho la hili tatizo," alisema.

Kadhalika, aliwataka makandarasi waliopewa kujenga barabara ya lami wilayani humo kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo kwa wakati, ili iwahudumie wananchi wa Loliondo, ambao hawakuwahi kupata barabara ya lami kwa miaka mingi.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Rashid Taka, aliishukuru serikali kwa uamuzi wa kujenga barabara hiyo kwa fedha za ndani, lengo ikiwa ni kuwaondolea adha wananchi wake, huku akiwataka wananchi kushughulika na maeneo korofi, ili wananchi wasafiri na kusafirisha mahitaji yao bila kukwama.

Meneja wa Tanroads Mkoa wa Arusha, Mhandisi John Kalupale, alisema kuwa wameanza kufanya usanifu wa maeneo korofi ya mito na mabonde makali, ili kuona uwezekano wa kuyakarabati na kuyaweka katika hali nzuri.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Zelothe Steven, aliwataka wananchi kushirikiana na makandarasi katika kutekeleza mradi huo na kuulinda, kwani umejengwa kwa nguvu za wananchi na kodi zao.

Ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha imelenga kukagua miradi ya barabara, kutatua kero za makandarasi pamoja na kushauri namna bora ya kuboresha miundombinu ya barabara.



## Wataka kampeni ya homa ya ini

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WAKAZI wa vijiji vya Mlangoni na Wiri katika Kata ya Garagua, Wilaya ya Siha, wameitaka serikali kuchukua hatua za kuanzisha kampeni maalum ya uelimishaji kuhusu ugonjwa wa homa ya ini na namna unavyoambukiza, kwa kuwa wengi wao hawana taarifa sahihi.

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wakazi wa vijiji hivyo walikuwa wakijadili namna utoaji wa huduma hiyo unavyotekelezwa katika wilaya hiyo.

Elikanael Meena, mkazi wa Mlangoni, alisema mpaka sasa hawajui ugonjwa huo unaambukizwaje na hatua gani wananchi wanapaswa kuchukua ili kujikinga na maradhi hayo.

"Mimi nimesikia huko sokoni eti anayetaka kupima homa ya ini anatakiwa kwenda Hospitali ya Wilaya lakini kwenye hayo matangazo yao hawasemi homa ya ini ni nini na mtu unajikingaje au una madhara gani. Sasa ni vizuri wanaohusika waje na kampeni maalum katika kila kijiji ili wananchi waelewe sawa sawa," alisema Meena.

Kwa upande wake, Shadrack Eliangiringa, mkazi wa Wiri, aliiambia Nipashe kuwa: "Nimefuatilia kujua iwapo wananchi wanalifahamu hili au wanaufahamu ugonjwa huu sambamba na hatua zake. Jibu la haraka nililolipata ni hapana."

Kwa upande wake, Anania Mollel, mkazi wa Mawasiliano, alisema ili wananchi waweze kujinusuru na ugonjwa huo, kuna haja ya elimu kuendelea kutolewa na watoa huduma ya afya kila mara ili kujenga uelewa wa namna ya kujikinga.

Akizungumzia zaidi Mollel alisema: "Siku chache zilizopita, nilibahatika kuzungumza na daktari mmoja wa Hospitali ya Rufani ya Mawenzi, angalau mimi alinipa elimu na ufafanuzi juu ya ugonjwa huu, dalili, ueneaji na jinsi ya mtu anayoweza kujikinga asiweze kuugua."

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, virusi vya ini viko katika makundi mbalimbali ambayo ni Hepatitis A, Hepatitis B, Hepatitis C na Hepatitis D.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao kila mmoja aliishauri Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuanzisha kampeni maalum ya kitaifa ambayo itakayotumika kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara na tiba dhidi ya ugonjwa wa homa ya ini (Hepatitis B).

Alipotafutwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Siha, Dk. Andrew Method, kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kuhusiana na ugonjwa huo na kama kuna zoezi la upimaji na utoaji wa chanjo linafanyika, hakupatikana kutokana na simu yake kuita bila majibu.

# Anayedaiwa kudai rushwa ya ngono kuajiri matatani

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WANAWAKE 22 wanaofanya kazi na kampuni moja iliyoko Wilaya ya Hai, wamefichua tuhuma nzito za kigogo wa juu wa kampuni hiyo kutaka rushwa ya ngono ili awatengenezee mazingira mazuri ya kuajiriwa.

Tuhuma hizo ziliibuliwa juzi na wafanyakazi wa kampuni hiyo, baada ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kukutana na wafanyakazi hao kusikiliza kero zinazowakabili.

Baada ya Ole Sabaya kuelezwa tuhuma hizo na wafanyakazi, aliagiza polisi wilayani humo kumtafuta na kumkamata mtuhumiwa anayelalamikiwa kuomba rushwa ya ngono.

"OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) mkamateni huyo bwana wanayesema ni Ofisa Uhusiano na mumkabidhi Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa). Haiwezekani alalamikiwe na wanawake 22 kuhusu tuhuma za ngono.

"Watu 22 wanawezaje kukutuhumu mtu mmoja kwamba unawataka kimapenzi na wameandika barua," alihoji Mkuu huyo wa Wilaya.

Aidha, inaelezwa kuwa kiongozi huyo wa ngazi ya juu ambaye ni Ofisa Uhusiano wa Kampuni (jina limehifadhiwa), huwalazimisha wanawake anaowataka kufanya naye mapenzi na kwa anayekataa, amekuwa akiwanyanyasa na kuwajengea mazingira ya kufukuzwa.

Kabla ya Ole Sabaya kuamuru kutiwa mbaroni ofisa huyo, awali wafanyakazi wa kampuni hiyo walitoa malalamiko yao yaliyosomwa na mwenzao.

Katika malalamiko yao, pia wafanyakazi hao wamedai kuwa wamekuwa wakicheleweshewa stahiki zao za mishahara, kufukuzwa kazi bila kufuatwa kwa utaratibu na hata bila mwajiri kupata taarifa.

Akiwasilisha malalamiko hayo mwakilishi wao alidai: "Huyo ofisa amekuwa akituhumiwa na wafanyakazi wenzetu ambao ni wanawake wanaofanya kazi hapa, kwamba amekuwa akiwanyanyasa na kuwataka kingono.

Pia amekuwa ni mtu wa kuchonganisha wafanyakazi na viongozi."

Kwa mujibu wa sheria, kosa hilo ni kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Makosa ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Namba 11 ya Mwaka 2007.



Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Daud Mayeji, akitoa taarifa kwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (wa tatu kulia), kuhusu mikakati ya jiji hilo, kukabiliana na changamoto za wanafunzi 18 wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Watumishi waonevu watangaziwa kibano

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI imesema haitakuwa na jicho la 'kengeza' katika kusimamia haki kama itabaini kuna baadhi ya watumishi wa umma, wanaotoa maamuzi ya kumwonea mwananchi wakati wa kushughulikia kero zinazowasilishwa kwao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alipokuwa akizungumza na wakuu wa idara, maofisa watendaji wa kata na vijiji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

"Endeleeni kutafuta haki za wananchi waliodhulumiwa, toeni maamuzi ya haki na msimwonee mtu. Wale watakaoona hawakutendewa haki wakija kwetu tutaangalia kama mmewaonea, lakini kama mmesimamia haki sisi kama Tamisemi tutawaunga mkono," alisema Waitara.

Waitara alisema Tamisemi inaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na viongozi mbalimbali hususan Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, kwa nia yao ni kumaliza matatizo ya wananchi katika ngazi husika.

Aidha, aliwashauri viongozi na watumishi wa wilaya hiyo kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria na taratibu, badala ya kuingiza hisia au kupendelea wala kumuonea mtu yeyote. Awali Mkuu wa Wilaya hiyo, Ole Sabaya, alimweleza Waitara kwamba wilaya hiyo inaendelea na kazi ya kutatua changamoto za wananchi kwenye masuala ya ardhi, ushirika na aina nyingine za madhila ikiwamo kuondoa matabaka miongoni mwa wananchi.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Hai, Dk. Irene Haule, akizungumza katika mkutano huo alimweleza Naibu Waziri huyo kuwa wilaya hiyo ikishirikiana na vyama vya ushirika imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Longoi kinachojengwa katika Kata ya Mnadani.

Kituo hicho kitahudumia wananchi wa kata za Masama Rundugai, Weruweru na Mnadani zenye wakazi zaidi ya 30,000 na kitakuwa na uwezo wa kutoa huduma zote za kawaida na dharura.

NIPASHE JUMATATU JANUARI 13, 2020

Nipashe
# Spotika



MAKOCHA 10 BORA LIGI KUU ENGLAND UK. 20



## ISIKUPITE

MCHEZAJI Bora wa Afrika wa mwaka 2019, Sadio Mane alizaliwa Aprili 10, mwaka 1992 na alifunga bao lake la kwanza la Ligi Kuu England Oktoba 18, mwaka 2014 akiwa na Southampton. Hat-trick ya kwanza ya mshambuliaji huyo aliifunga akiwa na klabu hiyo ndani ya dakika 2:56 katika ushindi wa mabao 8-0 dhidi ya Sunderland. Alitua Liverpool mwaka 2016 kwa dau la pauni milioni 34 akiwa mchezaji huru.

# NINACHOMOKA

Mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya kiungo wa Norwich, Todd Cantwell katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. United ilipata ushindi wa mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**



# HATIMA YA VALVERDE NA UJIO WA KOEMAN, XAVI BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

HALI si shwari ndani ya Barcelona kwa sasa, kwani ni wazi mashabiki na wapenzi pamoja na baadhi ya viongozi wanaona huu ni wakati mwafaka kwa kocha, Ernesto Valverde kuondoka klabuni hapo.

Valverde anakabiliwa na tishio la kufukuzwa nafasi yake hiyo baada ya kutokuwa na mwenendo mzuri.

Kipigo cha Alhamisi iliyopita dhidi ya Atletico Madrid kwenye nusu fainali ya Kombe la Mfalme Hispania, kinazidi kumweka kwenye nafasi mbaya.

Msimu huu unaonekana unaweza kuwa wa mwisho pale katika dimba la Camp Nou huku Ronald Koeman ndiye anayetajwa kuwania nafasi yake.

Barca walifungwa mabao 3-2 na Atletico kwenye nusu fainali ya Supercopa, kwa kuruhusu mabao mawili ya haraka dakika za mwisho huko Saudi Arabia, Alhamisi iliyopita.

Mabao kutoka kwa Lionel Messi na Antoine Griezmann yalisawazisha lile la mapema la Koke alilofunga dakika ya 46 hadi Barca walipofungwa mabao mawili ndani ya dakika tisa za mwisho na kuipa ushindi Atletico inayokwenda kuvaana na Real Madrid.

Kwa mujibu wa El Larguero na Cadena SER, Valverde ataendelea kuinoa timu hiyo hadi mwishoni mwa msimu huu, huku akipigiwa zaidi chapuo na Rais Josep Maria Bartomeu.

Lakini kwa upande mwingine kocha wa sasa wa Timu ta Taifa ya Uholanzi na gwiji wa Barcelona, Koeman ndiye anayepigia chapuo la kupewa mikoba hiyo.

Koeman alikuwa nyota pale Camp Nou akiwa mchezaji na alifunga bao la ushindi wa Kombe la Ulaya mwaka 1992.

Alikuwa na mafanikio mazuri kwenye nafasi yake ya ukocha akiwa pale Everton kwenye Ligi Kuu na pia alifanya makubwa pale Southampton na pia ameziongoza kwa mafanikio Ajax na PSV Eindhoven.

Hata hivyo, Barcelona italazimika kusubiri hadi baada ya michuano ya Euro 2020 ili kuweza kumpa nafasi hiyo.

**Xavi**

Wakati huo huo, maofisa wa Barcelona wameripotiwa kwenda nchini Qatar kwa ajili ya kuzungumza na gwiji wa klabu hiyo, Xavi ambaye naye anatajwa kutaka kupewa nafasi ya Valverde.

Baada ya kuondoka Barcelona mwaka 2015, Xavi alitumia miaka minne kama mchezaji akiwa na klabu ya nchini Qatari ya Al Sadd, kabla ya kuchukua mikoba ya ukocha Mei mwaka 2019.

**Suarez amtetea**

Luis Suarez amesema kwamba, kocha aliyekalia kuti kavu Barcelona, Valverde sio wa kulaumiwa kwa timu hiyo kutolewa kwenye nusu fainali ya Kombe la Supercopa de Espana dhidi ya Atletico Madrid.


Matokeo hayo yamezidi kuleta sintofahamu kuhusu majaliwa ya kocha, Valverde, lakini Suarez amemtetea kocha huyo mwenye umri wa miaka 55.

"(Valverde) sio wa kulaumiwa, makosa yalikuwa ya kwetu na sisi ndio tuliosababisha," alisema Suarez akiwaambia waandishi wa habari.

"Sijui kama kipigo hicho kitatusaidia sisi kukua, lakini kipigo hiki kinaonyesha tunatakiwa kujirekebisha mahali fulani.

"Inaonyesha kwamba, kuna makosa ambayo tunaweza kuyafanya na tukashindwa kabisa kuyasahihisha, lakini hili ni somo zuri kwetu."

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa zamani wa Timu ya Taifa ya Senegal, El Hadji Diouf (38), ambaye alikuwa Mwanasoka Bora wa Afrika mwaka 2001 na 2002, aliichezea Leeds United mechi 57 na kufunga mabao saba katika misimu miwili aliyoitumikia klabu hiyo.

# MICHEZO




Straika wa Simba John Bocco akijaribu kumtoka beki wa Yanga, Andrew Vicent 'Dante' kwenye mechi ya Ligi Kuu kati ya timu hizo, iliyochezwa Januari 4 kwenye Uwanja wa Taifa na kutoka sare ya mabao 2-2.

# REKODI 5 KALI MECHI ZA SIMBA, YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE mechi ya watani wa jadi kati ya Simba na Yanga iliyokuwa inasubiriwa kwa muda mrefu ilimalizika kwa sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, hapo Januari 4 mwaka huu.

Yalikuwa ni mabao ya Meddie Kagere kwa mkwaju wa penalti na Deo Kanda kwa upande wa Simba, huku Mapinduzi Balama na Mohamed Issa 'Banka wakiifungia Yanga.

Lilikuwa ni pambano zuri kwa pande zote. Simba ikiwa bora kipindi cha kwanza na Yanga ikawa imara kipindi cha pili na kusababisha mashabiki wa pande zote mbili waliokuwa wakishuhudia uwanjani, kusikiliza kwenye redio na hata kuangalia kwenye televisheni, kupamba burudani ya aina yake.

Kila kitu kimezungumzwa na kuandikwa kuhusiana na mechi hiyo jinsi ilivyochezwa, lakini kuna vitu vilivyojificha ambacho si wengi wanavitambua.

Ni kawaida mechi kubwa za Simba na Yanga zinapochezwa kuacha rekodi na takwimu mbalimbali.

Mwandishi wa makala haya anakuletea baadhi ya rekodi na takwimu mbalimbali zilizowekwa kwenye mechi hiyo.

**1. Balama aweka rekodi ya Msuva Yanga**

Wafungaji wa magoli ya Yanga, Mapinduzi Balama na Mohamed Issa wamekuwa ni wachezaji wa kwanza wa Kitanzania kufunga magoli kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Simba na Yanga tangu mwaka 2017.

Kwa misimu miwili iliyopita hakuna mchezaji yoyote wa Kitanzania wa Yanga aliyefunga goli kwenye mechi ya watani ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mchezaji wa mwisho wa Kibongo kufanya hivyo alikuwa ni Simon Msuva aliyefunga goli Februari 16 mwaka 2017, Ligi Kuu msimu wa 2016/17, Simba ikishinda mabao 2-1, Msuva akifunga kwa penalti, Laudit Mavugo na Shiza Kichuya wakifunga kwa upande wa Simba.

**2. Kagere arudia ya kina Kichuya, Tambwe**

Straika Meddie Kagere ameweka rekodi ya kufunga mfululizo kwenye mechi ya watani wa jadi.

Ligi Kuu msimu uliopita, Kagere alifunga bao pekee, Simba ikishinda bao 1-0 kwenye mechi ya mzunguko wa pili, lakini kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza msimu huu, amefunga tena bao na kuweka rekodi iliyowahi kuwekwa na wachezaji Amissi Tambwe na Yanga na Shiza Kichuya wa Simba.

Tambwe alifunga goli Ligi Kuu msimu wa 2015/16, Yanga ikiifunga Simba mabao 2-0 Septemba 26, 2015, akafunga tena kwenye mechi ya mzunguko wa pili msimu huo huo, Yanga ikishinda tena mabao 2-0 Februari 20, 2016, lakini Tambwe huyo alifunga tena bao msimu uliofuata 2016/17, Oktoba Mosi, timu hizo zilipotoka sare ya bao 1-1.

Kichuya wa Simba naye alifunga mfululizo akianzia Oktoba Mosi 2016, msimu wa 2016/17, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 na akafunga tena mechi ya mzunguko wa pili msimu huo huo, Februari 26, 2017, Simba ikishinda mabao 2-1.

**3. Sare ya 2-2 baada ya miaka 11**

Simba na Yanga zimetoka sare ya kufungana mabao 2-2 baada ya miaka 11 kupita. Mara ya mwisho kutoka sare hiyo ya magoli ilikuwa Aprili 19, 2009, mechi ikichezwa kwenye uwanja huo huo wa Taifa jijini.

Magoli ya Simba yalifungwa na Ramadhani Chombo 'Redondo' na Haruna Moshi 'Boban', huku ya Yanga yakifungwa na Ban Mwalala na Jerry Tegete.

**4. Kanda aweka rekodi ya Pitchou Kongo**

Baada ya miaka 20, Mkongomani Kanda anafunga goli kwenye mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga.

Mara nyingi mechi za watani wa jadi zinatawaliwa sana na wachezaji kutoka mataifa ya Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi na hata Ghana kufunga magoli, lakini kwa miaka 20 sasa hakukuwa na mchezaji wa Kikongomani aliyefunga bao kwenye mechi hiyo.

Mara ya mwisho Mkongomani kufunga kwenye mechi ya 'dabi' akiwa ni Pitchou Kongo, Agosti 7, 2004, Simba ikiichapa Yanga mabao 2-1. Lilikuwa ni goli la kufutia machozi, kufuatia yake ya Simba yaliyofungwa na Shaaban Kisiga na Ulimboka Mwakingwe.

**5. Matola na SMG wakumbushia ya mwaka 2007**

Makocha wasaidizi wa timu za Simba na Yanga kwenye mechi ya Januari 4, Selemani Matola wa Simba na Said Maulidi 'SMG' wa Yanga walikuwa wachezaji wa timu hizo mbili kwenye mechi ambayo zilitoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Jamahuri mjini Morogoro na Simba kushinda kwa penalti 5-4.

Mechi hiyo ilichezwa Julai 8, 2007, ikiwa ni fainali ya ligi ndogo, kutafuta bingwa wa Tanzania Bara, kabla ya kuanza mfumo wa msimu unaoanzia mwezi Agosti kama Ligi za Ulaya ambao ulianza mwezi uliofuata mwaka huo huo wa 2007.

Matola alikuwa kiungo wa mkabaji wa Simba na SMG alikuwa winga wa kulia ya Yanga, timu zikaenda dakika 120 bao 1-1, la Simba ikifunga na Moses Odhiambo na SMG ambaye aliwahi kuichezea Simba kabla hajahamia Yanga, akiisawazishia na kwenda kwenye penalti.

Baada ya miaka 12, wachezaji hao wakakutana tena, lakini safari hii kila mmoja akiwa benchi kama kocha msaidizi wa timu zao hizo hizo.

## NJE YA UWANJA



RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia ameteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Maalum ya kufanyia marekebisho mfumo wa vyama vya mchezo huo vya Kikanda barani Afrika (AZA).

Kamati hiyo imeundwa baada ya kikao kati ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), Shirikisho la Afrika (Caf) na AZA kilichofanyika hivi karibuni jijini Zurich, Uswisi na kuongozwa na Rais wa Gianni Infantino.

Wajumbe wengine wa kamati hiyo itakayoongozwa na Rais wa Caf, Ahmad Ahmad ni Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Mouad Hajji, Mario Gallavotti kutoka Fifa na Rais wa Shirikisho la Soka Niger (NFA), Hamidou Djibrilla.

Spotika 17

Extra Time

# REKODI 5 ZA EPL

## MBIONI KUVUNJWA NA LIVERPOOL



**LONDON, England**

KWA uhakika mwaka 2019 ulikuwa ni mwaka wa kuvunja rekodi kwa Liverpool.

Taji la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya miaka 14, wakanyanyua Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia kwa mara ya kwanza kwenye historia yao na kuongoza msimamo wa Ligi Kuu England.

Vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp wanaonekana hawataki kabisa utani msimu huu. Wanaongoza ligi kwa tofauti ya pointi 13.

Liverpool, imeshikilia uongozi wa Ligi Kuu England kwa mwaka mzima bila kufungwa.

Majogoo hao wa jiji Liverpool, waliweka mwanya huo wa alama 13 baada ya wapinzani wake wa karibu Leicester na Manchester City kujipatia ushindi katika mechi za mwaka mpya.

Kikosi hicho cha Klopp kilishuka kwa alama mbili wakiwa na alama 58 badala ya alama 60 msimu huu.

Livepool wameshiriki mechi 37 bila kupoteza na wakajizolea alama 101 wakati huo ambapo walipoteza kwa magoli 2-1 msimu uliopita kwa mabingwa Manchester City walipokutana Januari 3, 2019.

Arsenal ambao walishiriki michezo 49 katika msimu wa mwaka 2003-04 na Chelsea kutoka mwezi wa Oktoba 2004 hadi Novemba 2005 ni miongoni mwa timu ambazo zimecheza mechi bila kushindwa kwa mwaka mmoja.

Liverpool ilishindwa nyumbani dhidi ya Wolves katika Kombe la FA Januari mwaka jana.

Pamoja na timu yao ya vijana chipukizi kupoteza kwa Aston Villa katika Kombe la Carabao mwezi uliopita.

Liverpool imepoteza mara mbili katika Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona katika nusu fainali ya mkondo wa kwanza kabla ya mkondo wao wa pili dhidi ya Napoli mwaka huu katika hatua ya makundi.

Licha ya kutofungwa, Liverpool haikushinda kombe lolote la nyumbani mwaka 2019.

Mafanikio yao yalikuwa katika mechi za kimataifa, kuwa klabu ya kwanza ya England kupata ushindi wa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Uefa Super waliolipata Agosti baada ya kuichapa Chelsea kwa mikwaju ya penalti na katika michuano ya kombe la klabu bingwa ya duniani ya Fifa.

Makala hii inakuchambulia rekodi 5 ambazo Liverpool wanaweza kuzivunja msimu huu kwenye Ligi Kuu England;

**USHINDI MFULULIZO NYUMBANI**

Uwanja wa Anfield umekuwa bora zaidi kwako hadi sasa, huku wekundu hao wakiwa hawajapoteza mchezo wowote wa Ligi Kuu tangu mwaka 2017. Kwa sasa rekodi hiyo inashikiliwa na Manchester City ambao walishinda mechi 20 mfululizo kwenye uwanja wao wa nyumbani msimu wa 2011/12.

Kwa sasa Liverpool wamebakiwa na mechi mbili kufikia rekodi hiyo wakiwa na mchezo dhidi ya Manchester United, Southampton na West Ham ambazo zitapigwa kwenye dimba la Anfield.

Kama vijana hao wa Klopp watashinda mechi zote tatu zijazo, wataweka historia yao.

**USHINDI MECHI NYINGI UGENINI**

Liverpool imeshinda mechi zake zote nane za ugenini msimu huu na wakiacha pointi moja tu kwenye uwanja wa Old Trafford dhidi ya Manchester United.

Kama wakishinda mechi tisa kati ya 10 zilizobaki za ugenini watafikisha mechi 17 kushinda ugenini moja zaidi ya Manchester City ambao waliweka rekodi hiyo msimu wa 2017/18.

**MECHI NYINGI BILA KUFUNGWA**

Liverpool haijafungwa tangu ilipopoteza kwa Manchester City Januari 2019. Kama wataendelea kucheza bila kufungwa hadi mwishoni mwa msimu, wataivunja rekodi ya Arsenal ambayo walicheza siku nyingi bila kufungwa. Arsenal kwa sasa wanashikiria rekodi ya kutofungwa kwa siku 537, na Liverpool wanaweza kuzima ifikapo Juni 23 mwaka 2020.

**POINTI NYINGI KWA MSIMU**

Wakiwa hawajapoteza mchezo wowote msimu huu, Liverpool wana nafasi kubwa ya kuweka rekodi hiii msimu huu. Manchester City waliweka rekodi ya kufikisha pointi 100 msimu wa 2017/18.

Kama Liverpool watashinda mechi zake zote zilizobaki wataweka rekodi ya kuchukua pointi 112.

**TAJI LA KWANZA LIGI KUU**

Bila shaka Liverpool haitakuwa timu ya kwanza kushinda taji la Ligi Kuu, lakini itakuwa ni mara yao ya kwanza kulibeba taji hilo kwa kipindi cha miaka 30.

Wekundu hao wapo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kulibeba taji hili msimu huu hasa kutokana na kuwa wapo kileleni mwa msimamo wa tofauti ya pointi 13.


JURGEN-KLOPP

## Nukuu

"Nina furaha sana na wakati huo huo ninajisikia furaha kushinda tuzo hii, ni siku kubwa kwangu, ninapenda kuwashukuru watu wote wa Senegal. Wamekuwa na mimi wakati wote, wamekuwa wakinihamasisha kufanya vizuri," **alisema Sadio Mane baada ya kutangazwa mshindi wa tuzo ya Mwanasoka Bora wa Afrika kwa mwaka 2019.**



"Baada ya kutua Manchester City, siwezi kuwa kocha wa United, kama ilivyokuwa siwezi kuwa Kocha wa Real Madrid, ni bora nikaishi Maldives kama sitapata ofa ya kuzinoa klabu nyingine, Maldives kwa sababu hakuna kozi ya mchezo wa gofu, lakini ni mahali pazuri tu," **Kocha wa City, Pep Guardiola alisema alipoulizwa kama kuna uwezekano siku moja akatua Old Trafford.**



" Wakati nilipoongeza mkataba wangu mwaka 2018, tuliweka makubaliano kama nitafikia malengo, majadiliano tayari yameshaanza, tulizungumza mwezi uliopita. Nakaribia kufikia malengo yangu na kuongeza mkataba, lakini tutathibitisha baada ya kusaini," **nyota wa Manchester City, Fernandinho alisema.**





Kiungo wa Simba, Muzamiru Yassin (katikati), akiwa amekabwa na mabeki wa Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

# MTIBWA NA KISASI CHA 2015 KWA SIMBA LEO?

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni Januari 13 kama leo kwenye Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar, mwaka 2015 ilipochezwa fainali ya Kombe la Mapinduzi kati ya Simba dhidi ya Mtibwa Sugar.

Leo imetimia miaka mitano kamili timu hizo zinakutana tena kwenye fainali ya mashindano hayo kwenye uwanja huo huo.

Simba imetinga fainali kwa kuichapa Azam kwa penalti 4-3 baada ya sare ya bila kufungana kwa dakika 90, Mtibwa Sugar nayo ikiingia kwa kuwaondoa Yanga kwa mikwaju 4-2, zenyewe zikitoka sare ya bao 1-1 dakika 90 za kawaida.

Kwenye mechi ya fainali 2015, Simba ilifanikiwa kutwaa Kombe la Mapinduzi kwa kuichapa Mtibwa Sugar kwa mikwaju 4-3, baada ya kutoka sare bila kufungana kwa dakika 90.

Penalti za Simba ziliwekwa wavuni na Awadh Juma, Hassan Kessy, Hassan Isihaka na Dan Sserunkuma na za Mtibwa zikitiwa kwenye kamba na Ally Lundenga, Shaaban Nditi na Shiza Kichuya ambaye msimu uliofuata alijiunga na Simba.

Leo Mtibwa Sugar itaingia na dhamira moja tu ya kulipiza kisasi cha kufunga kwenye fainali kwenye mechi hiyo.

Simba iliingia fainali baada ya kuichapa Polisi ya Zanzibar bao 1-0, huku Mtibwa Sugar ikiwaadhibu JKU kwa mikwaju 4-3.

Ikumbukwe kuwa JKU ilitinga hatua hiyo baada ya kuitoa Yanga kwenye hatua hiyo kwa kuichapa bao 1-0.

Timu hizo mbili leo zinaingia uwanjani zikiwa na sura nyingi tofauti za wachezaji ambao wamesajiliwa katika klabu hizo ndani ya miaka hiyo mitano.

Ni wachezaji wachache tu ambao wamebaki kwenye klabu hizo kama vile nahodha Shaaban Nditi , Dickson Daudi na Issa Rashid 'Baba Ubaya' kwa upande wa Mtibwa Sugar, Ibrahim Ajibu, Jonas Mkude, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' na Said Ndemla kwa upande wa Simba.

Simba yapania kulichukua mara ya tatu

Simba ambayo imeingia fainali kwa mara ya sita sasa, imepania kutaka kulichukua kombe hilo kwa mara ya tatu kwenye historia ya michuano hiyo.

Imelichukua kombe hilo mara mbili na kuishia fainali mara tatu.

Mwaka jana Simba ilitinga hatua ya fainali na ikafungwa mabao 2-1 dhidi ya Azam ambayo safari hii imetolewa hatua ya nusu fainali na timu iliyoifunga fainali mwaka jana.

Mara ya kwanza Simba kutwaa Kombe la Mapinduzi ilikuwa ni mwaka 2011 ilipowafunga mahasimu wao wakubwa Yanga mabao 2-0 yaliyofungwa na Patrick Ochan na Shija Mkina, kabla ya kuja kulitwaa tena 2015 ilipoichapa Mtibwa.

Mara tatu ambazo imefika fainali na kulikosa, ukiacha ya mwaka jana ilipofungwa mabao 2-1 dhidi ya Azam, Simba ilitinga fainali zingine mwaka 2014 ilipofungwa na KCC ya Uganda bao 1-0 na mwaka 2017 ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC.

Mtibwa nayo ilishawahi kulichukua

Labda wapo wanaodhani kuwa kama ikilichukua leo Mtibwa Sugar itakuwa ni mara ya kwanza na itakuwa imebahatisha, si kweli.

Mtibwa ilishawahi kutwaa kombe hilo mwaka 2010, ilipoifunga Ocean View bao 1-0 kwenye mechi ya fainali, ilikiwekwa wavuni na Zuberi Katwila ambaye baada ya miaka tisa, anarejea kwenye michuano hiyo akiwa Kocha Mkuu wa timu hiyo.

Ulikuwa ni mwaka mzuri na wenye mafanikio kwa Mtibwa kwani kwenye mechi ya nusu fainali iliisulubu Simba mabao 3-0, mawili yakifungwa na Dickson Daudi ambaye hadi leo yupo kwenye kikosi hicho, moja likiwekwa wavuni na Said Mkopi.

Mtibwa imefika fainali kwa mara ya nne sasa, mara moja ikitwaa kombe na ikalikosa kwenye hatua ya fainali mara mbili kabla ya fainali ya leo.

Mara ya kwanza ilikuwa ni 2015 ilipofungwa na Simba kwenye hatua ya fainali kwa penalti 4-3 na mwaka unaofuata pia ilifanikiwa kufika hatua ya fainali, lakini ikakumbana na kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa URA ya Uganda.

**NAJUA WAJUA**



RAIS wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), Gianni Infantino, ambaye alizaliwa Machi 23, mwaka 1970, ni rais wa tisa wa shirikisho hilo na aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mchezo huko Ulaya kati ya mwaka 2009 na 2016.

## SOKA

# MAJERUHI UNITED FURAHA KWA YOUNG




**MANCHESTER, England**

NI wazi kwamba, uhamisho wa Ashley Young kwenda Inter Milan unaweza kusubirishwa kwanza kwa sababu ya matatizo ya majeruhi yaliyopo katika kikosi cha Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amethibitisha.

Young alikuwa kwenye harakati za kuondoka hapo United na kwenda San Siro wakati huu wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 atakuwa huru mwishoni mwa msimu huu na inaeleweka wazi kwamba Inter ilikuwa tayari kulipa fedha kwa ajili ya kukamilisha usajili wa Young mwezi huu.

Lakini United italazimika kubadili uamuzi kwa ajili ya kukiimarisha zaidi kikosi chake, lakini Young licha ya kubakiwa na miezi sita kwenye mkataba wake wa sasa ni wazi atalazimika kubakia hapo Old Trafford kabla ya kujiunga na Inter kipindi cha majira ya joto.

Hata hivyo, inaeleweka kwamba, United haipo tayari kumwachia aondoke mwezi huu kutokana na kukabiliwa na majeruhi kwenye safu yake ya ulinzi.

Zaidi ni kwamba, anajulikana kama kiongozi wa wachezaji wenzake katika vyumba vya kubadilishia nguo.

“Ni majadiliano yangu binafsi na Ashley na kuona nini kitatokea,” alisema Solskjaer. “Hatuna wachezaji wengi ambao wako fiti na tayari tunahitaji kuwa na kikosi kipana uwanjani.

“Ni mmoja wa wachezaji wetu na nahodha wetu. Kuna uvumi mwingine, lakini naamini tutaweza kuukabili. Ashley ni mmoja wa wachezaji anayejielewa zaidi, pamoja na uvumi wote, lakini amekuwa kwenye msimamo mzuri.

“Sidhani kama kuna chochote kitakachobadilika kwa sasa.

“Amekuwa mchezaji mzuri zaidi kwa klabu hii na amekuwa nahodha mzuri mno msimu huu, ngoja tuangalie tutakuwa wapi Juni.”

Habari zaidi zinasema kwamba, United imeamua kumpa ofa Young ili asaini mkataba mpya kumshawishi kubakia hapo badala ya kwenda nchini Italia.

Gazeti la Daily Mail limeripoti kwamba, United imempa ofa ya miezi 12 ya kuongeza mkataba wake ambao utamfanya alipwe pauni 110,000 kwa wiki.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Young ameikataa ofa hiyo kutoka kwa United.

Kwa upande mwingine, Inter imetajwa kwamba ipo tayari kumpa Young mkataba wa miezi 18 ili aondoke Old Trafford.

United iliamua kumpa ofa hiyo ili kumzuia kutofanya makubaliano na klabu nyingine baada ya kubakiwa na miezi sita kama sheria za shirikisho la soka la kimataifa, Fifa, zinavyosema.

Young amekuwa akitajwa kuvutiwa mno na Antonio Conte ambaye anataka kumchukua akacheza katika Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na miamba Inter.

Zaidi ni kwamba, Inter inaonekana ipo kwenye nafasi nzuri ya kuwania taji la Ligi Kuu Italia msimu huu, hicho ndio kinachomvutia zaidi Young ambaye anataka kuwa kwenye timu yenye mataji msimu huu.

Conte kwa muda mrefu alikuwa akimwania Young; alitaka kumsajili wakati akiinoa Chelsea.

United bao wanaonyesha kutokata tamaa kwa Young, kwani wanaamini atasaini mkataba mpya kabla ya kipindi cha majira ya joto.

Young ni mmoja wa wachezaji kadhaa ambao walionekana kutaka kuondoka mwezi huu pale United pamoja na Marcos Rojo na Nemanja Matic ambao wanahusishwa na klabu kadhaa.

Alipoulizwa kama atamruhusu Young kuondoka kipindi hiki cha majira ya kipindi cha baridi, Solskjaer alisema: “Siwezi kusema ndio au hapana, lakini tutaangalia nini kitakachotokea.

“Tunafanyia kazi kikosi chetu kwa ajili ya kukiimarisha zaidi, lakini lolote linaweza kutokea.”

**NDANI YA 18**



TIMU ya Arsenal ambayo kwa sasa iko katika nafasi ya 10 katika msimamo wa Ligi Kuu England ndio inashikilia rekodi ya kucheza muda mrefu bila kufungwa. Iliwahi kucheza siku 537 bila ya kufungwa.



KWA uhakika mwaka 2019 ulikuwa ni mwaka wa kuvunja rekodi kwa Liverpool. Taji la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya miaka 14, wakanyanyua Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia kwa mara ya kwanza kwenye historia...

**Uk. 16-17**

# MAKOCHA 10 BORA LIGI KUU ENGLAND



Guardiola

**LONDON, England**

WAKATI Ligi Kuu England ikiendelea kuchanja mbuga huku timu zikipigana dimbani kuwania ubingwa, hapa tunawaangalia makocha 10 bora kwa msimu huu hadi sasa.

**10. ROY HODGSON**
**Klabu: Crystal Palace**
Hii ni klabu ya nyumbani kwake, baada ya kuwa nje ya soka kwa muda, akarudi tena mwaka jana na sasa mambo anaonekana kwenda sawa kwa upande wake.

Aliichukua klabu hii kutoka kwa Frank de Boer ambaye alitimuliwa baada ya kuwa na matokeo mabaya pale kwenye dimba la Selhurst Park. Na sasa ameiweka timu hiyo kwenye nafasi salama ikiwa katikati ya msimamo wa Ligi Kuu England.

**9. David Moyes**
**Klabu: West Ham United**
Moyes amerudi tena kwenye Ligi Kuu England akiwa na ari na hamasa kubwa. Baada ya kushindwa katika klabu za Manchester United na Sunderland sasa amechukua jukumu la kuwanoa wagonga nyundo hao wa jiji la London.

**8. Ralph Hasenhüttl**
**Klabu: Southampton**
Kwa wanaomjua vizuri Ralph Hasenhüttl jina lake lina heshima kubwa katika soka la Ujerumani. Kazi yake katika klabu za Ingolstadt na RB Leipzig kule Ujerumani ikamfanya apate nafasi pale kwenye 'chuo' cha kukuza vipaji vya Waingereza Southampton.

**7. Carlo Ancelotti**
**Klabu: Everton**
Amekuja England. Waingereza wanapenda kumuita, Don Carlo! Kwa sasa anajaribu kurudisha makali ya Everton, wasifu wake na mafanikio yake yanajulikana duniani kote.

**6. Chris Wilder**
**Klabu: Sheffield United**
Baada ya miaka kadhaa kutawala ligi ya chini, Wilder sasa yuko kwenye Ligi Kuu England na hayuko vibaya sana.

Klabu yake ya Sheffield United ni moja ya timu inayocheza kwa ufundi zaidi barani Ulaya na sasa wanawania nafasi ya kutaka kucheza Ligi ya Europa kwa mara ya kwanza baada ya kurudi Ligi Kuu.

**5. Jose Mourinho**
**Klabu: Tottenham Hotspur**
Tottenham ilionekana kuyumba chini ya kocha, Mauricio Pochettino na wakaamua kumpa mikoba hiyo Jose Maourinho. Anajulikana kwa mbinu zake na uwezo wake. Ana nafasi kubwa ya kuipaisha Tottenham.

**4. Nuno Espirito Santo**
**Klabu: Wolverhampton Wanderers**
Kocha huyo raia wa Ureno amekuwa na mafanikio makubwa zaidi na klabu ya Wolves, msimu uliopita aliiwezesha kumaliza ikiwa nafasi ya 7 kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kurudi kwenye ligi hiyo. Na pia wakafuzu kucheza Ligi ya Europa na hadi sasa inaonekana kuwa timu yenye upinzani mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England.

**3. Brendan Rodgers**
**Klabu: Leicester City**
Baada ya kushinda mataji mengi akiwa nchini Scotland na klabu ya Celtic, Rodgers akaamua kurudi kwenye Ligi Kuu England mapema mwaka 2019. Akapewa mikoba ya kuinoa Leicester na kwa uhakika ameiweka kwenye kiwango bora zaidi ikitoa upinzani mkubwa kwenye nne bora.

**2. Pep Guardiola**
**Klabu: Manchester City**
Pengine ni kocha bora zaidi kuanzia miaka ya 2010 na kwa uhakika anaendelea kuwa bora hadi miaka ya 2020. Guardiola alipofika England akatawala soka la Uingereza kwa miaka miwili mfululizo. Kwa sasa anaendelea kupambana kwenye Ligi Kuu England.

**1. Jurgen Klopp**
**Klabu: Liverpool**
Kwa sasa ndiye kocha bora katika Ligi Kuu England na Ulaya. Ameifanya Liverpool kuwa moja ya klabu bora zaidi barani Ulaya akibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kutinga fainali mara mbili.

Msimu huu 'njaa' yake kubwa ni kutaka kulibeba taji la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30.

## USILOLIJUA



TIMU ya Taifa ya Afrika Kusini (Bafana Bafana), ilicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa mwaka 1924, lakini ikafungiwa kwa miaka 16 na Fifa na baadaye ikasimamishwa na kuwa nje ya michuano kwa miaka 40 kutokana na kuwapo kwa vitendo vya ubaguzi wa rangi nchini humo.



# Wakuu wa shule, maofisa elimu wachangia vifaa shule

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKUU wa shule za sekondari na maofisa elimu wa Jiji la Mbeya, wamechangia vifaa vya kufundishia kwa ajili ya kuwezesha kufunguliwa shule mpya ya Sekondari ya Kata ya Mwasekwa.

Shule hiyo ilichangiwa Sh. milioni 10 na Rais John Magufuli wakati wa ziara yake mkoani Mbeya Aprili mwaka jana.

Baada ya kukamilika ujenzi wa shule hiyo, ilikabiliwa na ukosefu wa vifaa vya kufundishia wanafunzi, hali iliyosababisha isifunguliwe.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo kwa uongozi wa shule hiyo mwishoni mwa wiki, Ofisa Elimu Sekondari wa Jiji la Mbeya, Mwalimu Felix Danda, alisema vifaa vilivyochangwa na walimu hao vina thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10.

Alivitaja baadhi ya vifaa ambavyo vilichangwa na walimu hao kuwa ni vitabu vya masomo yote, vifaa vya maabara, kabati, karatasi za kuchapishia mitihani, kalamu za kuandikia, mifagio pamoja na ndoo za kufanyia usafi.

"Watoto waliofaulu na wanatakiwa kujiunga katika shule hii ni 62, vyumba vya madarasa vilikuwa vimekamilika kwa nguvu zenu wananchi, lakini vifaa vilikuwa havipo na tungeamua kuwachangisha tena ingekuwa tatizo ndio maana kila mwalimu aliona ni vema kuchangia," alisema Danda.

Aliwataka wazazi kuhakikisha wanawapeleka watoto wote waliochaguliwa kujiunga na shule hiyo hata kama hawana sare za shule kwa maelezo kuwa watapewa muda wa kununua sare hizo.

Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwashilindi, aliwashukuru wakuu hao wa shule za sekondari kwa michango waliyotoa kwenye shule hiyo.

Aidha, aliwataka wananchi wa Kata ya Mwansekwa kuhakikisha wanaitunza shule hiyo kwa kushiriki kuchanga michango mbalimbali kwa ajili ya kukarabati miundombinu.

Aliuomba pia uongozi wa shule hiyo kuhakikisha vifaa vya maabara vinatumika vizuri na kutunzwa ili vidumu na kuwasaidia watoto wengi zaidi katika kata hiyo.

"Ofisa Mtendaji hakikisha watoto wote waliofaulu wanaanza masomo, msako upite nyumba kwa nyumba na mzazi ambaye hatataka kumleta mtoto wake hapa ni lazima tushughulike naye, uzuri ni kwamba sasa hivi hakuna michango shuleni kwa hiyo hakuna kisingizio," alisema Mwashilindi.

Aidha, aliahidi kuchangia Sh. milioni 1.5 kwa ajili ya kusaidia kukamilisha baadhi ya miundombinu ambayo bado haijakamilika na akamtaka Ofisa Mtendaji kusimamia matumizi ya fedha hizo.

Akizungumza kwa niaba ya Maofisa Elimu wa Kata za Jiji hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iyela, Dickson Sinkwembe, aliwashukuru wadau wote wa elimu waliochangia michango yao katika shule hiyo.



Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza wa Shule ya Sekondari Mwansekwa ya jijini Mbeya, wakiwa wamebeba vifaa mbalimbali vya shule hiyo, baada ya gari iliyokuwa imebeba kushindwa kufika shuleni hapo, vifaa hivyo vilichangwa na wakuu wa shule za sekondari za Jiji la Mbeya na waratibu elimu wa kata ili kusaidia shule hiyo kufunguliwa. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

## Watakiwa kujiunga CHF uhakika matibabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Bonde la Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameshauriwa kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (CHF), ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mratibu wa CHF iliyoboreshwa katika bonde hilo, Abdul Yahaya, wakati wa mkutano wa kuhamasisha wananchi kujiunga na mfuko huo uliofanyika katika Mji wa Mbalizi.

Aidha, alisema gharama ya kujiunga ni Sh. 30,000 pekee kwa familia moja. Yahaya ambaye ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Bonde la Mbalizi, alisema mtu akijiunga na mfuko huo atapata matibabu yeye na familia yake isiyozidi watu sita kuanzia kwenye zahanati mapaka kwenye hospitali ya rufani ya mkoa.

Alisema wananchi wanatakiwa kuchangamkia fursa hiyo kwa madai kuwa magonjwa huwa hayapigi hodi na hivyo yanaweza yakamkuta mtu akiwa hana hela, lakini kama ni mwanachama wa mfuko huo lazima atatibiwa.

"Hakuna ambaye ana uwezo wa kutabiri kuwa ataugua siku fulani na akaandaa fedha kwa ajili ya matibabu, kwa sababu hiyo ndio maana tunahamasisha watu kujiunga na mfuko huu," alisema Yahaya.

Alisema wananchi wanaweza wakajiandikisha kwa kumtafuta yeye mwenyewe ama kwa viongozi wa mitaa yao ambao watawaelekeza mahali pa kujiandikisha.

Aliwataka wananchi wote ambao ni wanachama wa mfuko huo kuwasiliana na viongozi endapo wanakumbana na matatizo wakati wanaenda katika kituo chochote cha serikali cha kutolea huduma za afya.

# Mbunge atoa saruji 170 ujenzi madarasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, ametoa msaada wa mifuko 170 ya saruji kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule za Sekondari Usongwe na Malama zilizopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Msaada huo uliwasilishwa juzi na Peter Mtepa kwa niaba ya mbunge huyo ambaye alisema mifuko 100 ni kwa ajili ya Shule ya Sekondari Usongwe ambayo wananchi wanajenga vyumba vya madarasa tisa na mifuko 70 Shule ya Sekondari Malama.

Mtepa alisema mbunge huyo aliguswa kutoa msaada huo baada ya kuona wananchi wanajitolea nguvu zao kujenga vyumba vya madarasa bila kulazimishwa na hivyo akabaini kuwa wanamwitikio mzuri kwenye shughuli za maendeleo.

Aliwataka viongozi wa shughuli za maendeleo katika Kata za Utengule Usongwe na Kata ya Nsalala ambako shule hizo zinapatikana wasimamie ujenzi wa vyumba vya madarasa, ili vikamilike mapema na wanafunzi wa kidato cha kwanza waliokosa nafasi waanze masomo.

Akipokea mifuko 100 hiyo kwa ajili ya Shule ya Sekondari Usongwe, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mbalizi, Paulo Mwampamba, alisema wanafunzi 400 waliochaguliwa kidato cha kwanza katika shule hiyo ya Usongwe, wamekosa nafasi kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Alisema vinahitajika vyumba tisa ambavyo ndivyo vinaendelea kujengwa na kwamba mpaka kufikia Februari 15 mwaka huu, vitakuwa vimekamilika na wanafunzi hao wataanza masomo Februari 16 kama walivyoelekezwa.

Alisema kwa sasa mbali na mchango wa mbunge wa jimbo hilo, pia wapo wadau mbalimbali ambao wanaendelea kupeleka misaada shuleni hapo kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi ambao wanajitolea kujenga vyumba hivyo.

"Tumesaidiwa na wafanyabiashara wa mji wetu wa Mbalizi, Mkuu wa wetu wa Mkoa, Albert Chalamila ametuahidi bando 35 za mabati kwa ajili ya kuezeka vyumba hivi, wenzetu benki ya NMB pia wameomba watusaidie kuezeka vyumba hivi," alisema Mwampamba.

Alisema pia wananchi wa Kitongoji hicho wanachangia Sh. 3,000 kila mmoja pamoja na kujitolea kwenda kufanya shughuli za ujenzi kwa kubeba mawe, mchanga, kuchota maji na hata kuwasaidia mafundi.

Baadhi ya wananchi wa Kitongoji cha Mbalizi waliohudhuria kwenye shughuli za maendeleo katika Shule hiyo ya Usongwe waliiomba serikali kuwapelekea walimu shuleni hapo baada ya vyumba kukamilika ili watoto wao wasome vizuri.

Mmoja wa wananchi hao, Asha Masebe alisema wananchi wengi wanajitokeza kwenye maendeleo kutokana na watoto wao wengi waliofaulu kukosa nafasi.

Alisema lengo lao ni kukamilisha vyumba vya madarasa na hivyo akaiomba serikali na yenyewe kuandaa walimu pamoja na vifaa vya kutosha kufundishia, ili wanafunzi hao watakapoanza masomo wasipate shida.



# Tango, wabunge kuimarisha ushirikiano

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKISHO la Asasi za Kiraia (TANGO) limejipanga kuimarisha ushirikiano na wabunge, ili kuhakikisha wanafanikisha utendaji wao katika majimbo wanayotoka.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na Mkurugenzi Mtendaji wa Tango Ngunga Tepani, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na mikakati ya shirikisho kwa mwaka 2020.

Alisema lengo ni kuimarisha uhusiano baina yao na wabunge ili kurahisisha utendaji kazi wa kila mmoja katika eneo ambalo anatoka kulingana na majukumu yake. "Tumejipanga kuhakikisha mwaka huu tunaboresha uhusiano wetu lengo ni kuona kila mmoja anatekeleza jukumu lake ipasavyo katika eneo analotoka," alisema Tepani.

Aidha, alisema wamejipanga kwenye kila idara ili kuhakikisha wamefanikiwa mikakati waliojiwekea.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, wanatarajia kuunda tume ya pamoja itakayosaidia kutatua vikwazo vinavyopatikana katika utendaji kazi wao kuanzia ngazi ya chini hadi taifa.

Alisema wazo la kuanzisha tume ya pamoja lilitokana na mkutano uliofanyika Novemba mwaka jana, jijini Dodoma uliokuwa na lengo la kuzungumzia changamoto mbalimbali za utendaji kazi wa asasi za kiraia wanazokutana nazo.

"Tume hiyo ya pamoja itafanya kazi bila kujali ni maeneo gani inatakiwa kwenda kufanya kazi," alisema Tepani.

Aidha, alisema wamejipanga kuanzisha tovuti ili wabunge wapate taarifa zitakazowasaidia katika utendaji kazi zao wanapokuwa bungeni kuchangia mijadala inayowasilishwa ikiwamo kuwasilisha hoja za msingi bungeni.

Alisema lengo ni kuona ushirikiano unaimarika baina yao na wabunge kutokana na kwamba wote wanafanya kazi za kijamii kuhakikisha wananchi wananufaika na utendaji kazi wao wa kila siku katika majimbo yao.

Akizungumza kuhusu mpango mkakati ya mwaka huu, alisema wamejipanga kuhakikisha wanakuwa na mikutano ya mara kwa mara ili kufanikisha malengo waliojiwekea kwa mwaka 2020.

Mkurugenzi huyo, aliwaomba wabunge kuendelea kushirikiana pamoja ili kufanya kazi kwa pamoja lengo ikiwa ni kuisaidia serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.



Mbunge wa Sikonge, Joseph Kakunda, akichangia hoja wakati wa mkutano wa Baraza la Madiwani la kujadili na kupitia mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya mwaka 2020/21. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara Dodoma watakiwa kuwa wabunifu

**Na PeterMkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa samaki wabichi, mboga na matunda katika Soko la Bonanza Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wametakiwa kuacha kufanya biashara kwa mazoea badala yake waboreshe ili waweze kufikia malengo na kujikwamua kiuchumi.

Aidha, wametakiwa kutumia fursa za ukuaji wa kasi wa Jiji la Dodoma kutokana na serikali kuhamia huko, kwa kuwa kuna idadi kubwa ya watu wanaoweza kununua bidhaa zao.

Ushauri huo ulitolewa hivi karibuni na Mwenyekiti wa soko hilo, Marwa Mabucha, wakati akizungumza na wafanyabiashara baada ya kuchaguliwa kwenye uchaguzi mkuu wa viongozi wa soko hilo uliofanyika jijini Dodoma. Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kuachana na biashara za mazoea ambazo hazina tija, badala yake wafanye kwa malengo ya kuinua mitaji yao ili waweze kupata mikopo ambayo itawawezesha kukabiliana na wingi wa wateja wanaowahudumia.

Mabucha alisema bila wafanyabiashara wakabadilisha mtizamo wao wa kizamani wa kufanya biashara kimazoea kwa idadi ile ile ya watu na wakati ikiwa Manispaa hawataweza kujiinua kiuchumi na kuendana na mahitaji.

Mwenyekiti huyo ambaye alichaguliwa kwa kura 196, aidha aliwataka wafanyabiashara hao kushirikiana kwa pamoja na Halmashauri ya Jiji ili kuweza kuboresha soko hilo kwenye miundombinu.

Kwa upande wake mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Goya Magwai, aliutaka uongozi uliochaguliwa kushirikiana na wafanyabiashara hao pamoja na Jiji ili waweze kuwahudumia wateja wao na kutatua changamoto zilizopo. Katika uchaguzi huo viongozi wengine waliochaguliwa ni pamoja na Makamu Mwenyekiti Fortunatus Keleta, aliyechaguliwa kwa kura (119), Katibu wa soko Dickson Mwesigwa (209), Katibu Msaidizi Hamisi Mbula (105) na Mtunza Hazina Elias Manikulu (286).

# Wazazi watakiwa kulinda watoto

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAZAZI wanaoishi kandokando na maeneo ya Makorongo yanayotiririsha maji wametakiwa kuwa makini na watoto wao ambao wanakwenda eneo hilo la kuvua samaki aina ya kambale.

Rai hiyo ilitolewa na Diwani wa Viti Maalum Kata ya Iloje, Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Hilda Kadunda (CCM), alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu madhara yanayoweza kujitokeza iwapo wazazi hawatakuwa makini na watoto wao.

Diwani huyo alisema kuwa kwa kipindi ambacho mvua inaendelea kunyesha maji mengi yanatoka katika Bwawa la Mtera na kuingia kwenye makorongo mbalimbali yakiwa na samaki hao aina ya kambale.

Aidha, alisema kwa sababu hiyo jamii kubwa utumia fursa hiyo kuvua kwa njia ya kutumia rungu kwa lengo la kujipatia mboga na wakati mwingine kujiongezea kipato.

Alisema kipindi cha uvuvi kuna msemo wa "Mtaji Rungu" kwa maana ya kila mmoja anaweza kumvua samaki aina ya kambare kwa kutumia rungu kumpiga kichwani hutumika.

Alisema kazi hiyo ni hatari kwa watoto ambao wanalazimika kuingia kwenye maji yanayotembea.

"Wakati wa kipindi cha mvua kama hiki maji mengi hutoka bwawani na kuingia katika makorongo, maji hayo huwa na samaki wengi aina ya kambale, jamii ya huku kwa kuwa ni wavuvi utumia fursa hiyo kuingia kwenye makorongo kwa kutumia rungu kwa ajili ya kuvua samaki hao.

"Uvuvi husaidia jamii kupata mboga na wakati mwingine kupata samaki wengi ambao wanawaingizia kipato kwani upatikana samaki wa kutosha hadi kufikia hatua ya kuweza kuwabani na kuwasafirisha hadi Dodoma Mjini au hata mikoa ya nje ya Dar es Salaam," alisema.

"Samaki huvuliwa kwenye mkondo wa maji ambayo ni mengi na wakati mwingine yanakuwa na kasi kubwa ndiyo maana nawasisitiza wazazi na walezi wawe makini kwa kutowaruhusu watoto ambao hawawezi kuhimili nguvu ya maji kuingia kuanza kujihusisha na uvuvi wa samaki hao kwani inaweza kujitokeza madhara hapo baadaye," alieleza Diwani Hilda.



# JPM akerwa matokeo mabaya shule za Znz

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS Dk. John Magufuli amesema kuwa haridhishwi na matokeo ya mitihani ya taifa ya kidato cha nne na sita kwa Zanzibar kutokana na shule nyingi kushika nafasi za mwisho.

Aliyasema hayo juzi wakati akiweka jiwe la msingi katika Shule ya Sekondari Mwanakwerekwe Mjini Unguja.

Rais Magufuli aliwataka walimu kuongeza bidii na kuhakikisha kwamba ufaulu mzuri wa wanafunzi unapatikana.

"Hili nitalisema, ingawa najua wengine hawalifurahii....ni aibu kuona shule kutoka Zanzibar zinashika nafasi za mwisho katika mitihani ya taifa," alisema.

Aidha, Rais Magufuli alimtaka mkandarasi wa shule hiyo kampuni ya CRJ kumaliza mradi kwa wakati kwa mujibu wa mkataba uliofikiwa wa Machi mwaka huu na kuacha visingizio visivyokuwa na sababu.

Alisema hakubaliani na maelezo ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya kusema kwamba mradi huo umechelewa kwa sababu ya mvua nyingi zilizonyesha katika kipindi kirefu pamoja na uhaba wa mchanga.

"Mimi sikubaliani na kisingizio hicho cha mvua nyingi kunyesha katika kipindi kirefu cha mwaka mzima...kwani kule Ulaya hakuna mvua na kila siku wanajenga majengo makubwa," alisema.

Alisema fedha za ujenzi wa shule hiyo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, hivyo unatakiwa kulipwa kwa fedha za walipakodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli alisema Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 1964 yamefungua mafanikio ya sekta mbali mbali ikiwamo elimu ambayo kabla ya hapo ilikuwa ikitolewa kwa misingi ya ubaguzi.

Alisema mafanikio hayo yamekuja baada ya serikali kuweka kipaumbele katika sekta ya elimu kwa kuwapatia wanafunzi elimu bure kuanzia maandalizi, msingi hadi sekondari.

Alieleza kabla ya Mapinduzi elimu ilikuwa ikitolewa kwa misingi ya ubaguzi kwa matabaka machache ndiyo yaliyokuwa yakifaidika.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza misingi ya kutoa elimu bure kama ilivyoasisiwa na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume.

Alisema sekta ya elimu imepiga hatua kubwa baada ya Mapinduzi ambapo elimu ya maandalizi, msingi na sekondari inatolewa bure kwa watoto wote bila ya ubaguzi.

Alisema idadi ya wanafunzi wa elimu ya maandalizi imeongezeka kutoka 238 hadi 382,wakati wanafunzi wa msingi wameongezeka kutoka 299 hadi 381, huku idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu ikiongezeka na kufikia 3,624 pamoja na idadi ya vyuo vikuu.

"Hayo ni mafanikio makubwa ambayo tunastahiki kujivunia kwa sababu yameleta maendeleo makubwa katika sekta ya elimu na kuongeza idadi ya wahitimu," alisema.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, aliipongeza Benki ya Dunia kwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa shule za ghorofa zinazoendelea kujengwa Unguja na Pemba.

Alisema ujenzi wa shule hiyo ni utekelezaji wa mradi wa kuinua uwezo wa wanafunzi wa shule unaotekelezwa na Benki ya Dunia na kuzihusisha jumla ya shule 22. Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Idrissa Muslim Hijja, alisema mradi huo utahusisha shule 22, na kwamba utagharimu jumla ya Sh. bilioni 80.



Wananchi wakipita kwenye maandamano mbele ya jukwaa kuu wakitoa heshima kwa Dk. Shein katika sherehe za Miaka 56 ya Mapinduzi kwenye Uwanja wa Amaan jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Shein asamehe wafungwa 19

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ametoa msamaha kwa wafungwa 19 ambao bado walikuwa wakiendelea kutumikia vyuo vya mafunzo (magereza) vya Unguja na Pemba ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, Rais Shein amefanya hivyo kutokana na uwezo aliopewa chini ya kifungu cha 59 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa, kwa kuwa Zanzibar inasherehekea Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kuwa Rais ameridhika kuwa kuna sababu za kutosha za kutumia uwezo wake huo katika sherehe hiyo, wafungwa hao waachiwe huru.

Walionufaika na msamaha huo kwa Unguja ni Salum Kombo Juma, Rashid Abdalla Salum, Shaame Mussa Suleiman, Rajab Juma Suleiman, Mwinyi Abdalla Rajab, Faki Ramadhan Juma, Abdalla Said Khamis, Omar Khalfan Said, Abdulbaki Abdulaziz Muhammad, Mwinyi Maulid Haji, Said Ali Seif na Abdalla Ame Khamis.

Wengine walionufaika na msamaha huo kwa upande wa Pemba ni Fauzi Abdalla Said, Is-haka Saleh Ali, Hashim Moh'd Khamis, Ussi Juma Khamis, Juma Salum Moh'd, Moh'd Khamis Ali na Maulid Abdalla Seif.

Msamaha huo ambao hutolewa kila mwaka katika kipindi cha sherehe za Mapinduzi, huwahusisha wafungwa ambao ni wazee sana, wenye maradhi sugu au wenye makosa madogo ambao wamebakisha muda mfupi wa kutumikia sambamba na kuonyesha nidhamu nzuri na kujutia makosa yao.

Wafungwa wa Magereza, wenye makosa ya kuua kwa makusudi, wizi wa kutumia nguvu, wizi wa mali ya umma, makosa ya kudhalilisha wanawake na watoto, makosa ya dawa za kulevya na wenye makosa mengi ya zamani kwa kawaida huwa hawapewi msamaha.

# ...Akunwa na uwekezaji wa wazalendo

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS John Magufuli amesema serikali itawaunga mkono wafanyabiashara wazalendo wenye nia ya kuwekeza miradi ya maendeleo itakayokuza pato la taifa kiuchumi.

Alisema hayo wakati akifungua hoteli ya Verde yenye hadhi ya nyota tano iliopo eneo la Mtoni nje kidogo ya mji wa Unguja.

Alisema mfanyabiashara Said Salim Bakhressa ni wa kupigiwa mfano ambaye ameamua kutumia fedha zake kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wazalendo kwa kuwekeza. Alikemea tabia ya baadhi ya watendaji serikalini kuwakatisha tamaa wafanyabiashara wazalendo walioonyesha moyo wa kuwekeza.

"Nawataka watendaji wetu kuacha tabia ya kuwakatisha tamaa wafanyabiashara wazalendo... wekezeni nchini na muache tabia ya kuficha fedha nje ya nchi ukifa zitaliwa na watu wengine," alisema. Aliwataka wafanyabiashara wengine kuiga mfano wa Bakhressa wa kuwekeza kwanza nchini na baadaye kuwekeza nchi jirani.

"Nilipokwenda Malawi niliambiwa yupo mwekezaji Bakhressa... ukienda DRC Congo yupo...huo ndiyo uwekezaji tunaoutaka baada ya kujitosheleza kuwekeza nchini," alisema.

Magufuli alitoa changamoto kwa taasisi zinazofanya kazi katika kutangaza utalii Zanzibar na Tanzania Bara kushirikiana ili kuitangaza sekta hiyo.

Alisema Tanzania Bara kwa mwaka imepokea watalii milioni 1.5,wakati Zanzibar imepokea watalii 520,809 katika mwaka 2018.

Hata hivyo, alisema idadi ya watalii wanaotembelea katika nchi mbili za Misri na Morocco wanafikia kwa mwaka milioni 10.

"Tunahitaji kushirikiana zaidi katika kutangaza utalii ...kipo kisiwa kidogo cha Maldive kinapokea watalii milioni 1.5 kwa mwaka," alisema. Mwakilishi wa mwekezaji wa kampuni ya Bakhresa Group, Salim Aziz, alisema ujenzi wa hoteli hiyo ni mkopo kutoka Benki ya Exim ambao umetoa jumla ya ajira 250, huku wakiwamo watu wenye ulemavu 16.

Alisema ujenzi wake ulianza mwaka 2015, huku ukijikita zaidi katika kulinda na kuhifadhi mazingira ya aina mbalimbali yakiwamo ya bahari ambapo eneo la hekta 10 limefukiwa bahari.

Alisema hoteli ya Verde imechangia kodi serikali kuu jumla ya Sh.bilioni 4 tangu ilipoanza kutoa huduma baada ya kuwekwa jiwe la msingi mwaka 2016.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Khamis Mussa, alisema mwekezaji ameonyesha uzalendo wa hali ya juu kwa kuwekeza Zanzibar katika miradi mbalimbali.

# Watendaji wapewa angalizo kuhujumu mapato

**Na Gurian Adolf**, NKASI

WILAYA ya Nkasi mkoani Rukwa imewaonya watendaji kuacha tabia ya kuhujumu mapato kwa kujinufaisha wao kwani tabia hiyo, itasababisha wengi wao kupoteza ajira kwani hawatavumiliwa kuachwa waendelee kufanya vitendo hivyo.

Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, ndiye aliyetoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki katika kikao cha Baraza la Madiwani kwa lengo la kupitisha bajeti ya Sh. bilioni 29 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Alisema kuwapo baadhi ya watendaji wa serikali ambao wamekuwa vinara katika vitendo vya kuihujumu serikali kwa kuiibia mapato kitendo ambacho ni kibaya na hakitavumiliwa badala yake watendaji hao watafukuzwa kazi, kwani halmashauri hiyo haipo tayari kushuhudia vitendo hivyo vikiendelea kutokea.

Akitolea mfano katika mwaka wa fedha uliopita, alisema kuwa kuna watendaji wa Idara ya Misitu wa halmashauri hiyo walikamata ng'ombe wa wafugaji wanne na ilipaswa wawalipishe wafugaji hao faini ya Sh. 10,000,000 kila mfugaji ambapo halmashauri ingepata Sh. 40,000,000 lakini wao walipunguzia na kuwatoza Sh. 6,000,000 kila mfugaji na fedha hizo walizichukua wao badala ya kuwa ni makusanyo ya halmashauri.

Mtanda alisema watumishi hao walikamatwa na kukabidhiwa Takukuru ambapo uchunguzi unaendelea, hivyo kuwataka watumishi wa umma kuacha tabia za kuhujumu mapato ya serikali kwani ni mbaya na itawatokea puani.

Awali, akiwasilisha bajeti hiyo mkurugenzi mtendaji wa halmashauri hiyo Misana Kwangula alisema kuwa katika bajeti hiyo fedha kutoka serikali kuu ni Sh. bilioni 26 mapato ya ndani, yatakuwa ni Sh. bilioni 2.489 na michango ya wananchi itakuwa ni Sh. milioni 670.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Zeno Mwanakulya, aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kuwa mstari wa mbele katika maeneo yao kwa kuhakikisha kuwa makusanyo yanapatikana na wanawasimamia watendaji ili wahakikishe wanafanya kazi hiyo katika misingi inayokubalika.

Naye Diwani wa Chala, Michael Mwanalinze, aliomba halmashauri hiyo kuhakikisha kuwa makusanyo ya ndani yawe yarudishwa kwenye miradi iliyoanzishwa na wananchi ili waone namna wanavyonufaika na mapato wanayotoa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene (kulia), akimsikiliza mmoja wa watendaji wa kiwanda cha kuzalisha nondo cha Fujian Hexingwang Industry kilichopo Kisemvule Mkoa wa Pwani, kabla ya kukifungia kwa kipindi cha mwezi kwa kusababisha uchafuzi wa mazingira katika makazi ya watu na kukiuka sheria na kanuni za mazingira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Madaktari bingwa magoti, nyonga kutoa huduma Dar

**Na Mwandishi Wetu**

MADAKTARI bingwa wa upasuaji wa nyonga na magoti kutoka India, wanatarajiwa kuwafanyia uchunguzi na upasuaji watu wenye matatizo hayo nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Hospitali ya Regency, uchunguzi wa magonjwa hayo utafanyika kuanzia Januari 23, hadi 25 mwaka huu katika hospitali hiyo jijini Dar es Salaam.

Ilisema ujio wa mtaalamu huyo utapunguza gharama za wagonjwa kwenda nje ya nchi kufuata tiba hiyo.

"Katika jitihada za kupunguza rufani za wagonjwa kwenda matibabu nje ya nchi na kuokoa fedha nyingi za kigeni ambazo zimekuwa zikitumika tumeona ni vyema kuita mara kwa mara mtaalamu huyu kufanya upasuaji hapa Dar," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema ujio wa mtaalamu huyo umekuwa ukisaidia kuwapa ujuzi wataalamu wa ndani ili mwishowe wawe na utaalamu wa kufanya upasuaji wa aina hiyo wao wenyewe.

Aidha, ilisema mpango wa kuita madaktari hao bingwa wa magoti na nyonga umekuwa ukiratibiwa na Hospitali ya Regency kwa kushirikiana na Hospitali ya HCG Multi-Specialty iliyoko mji wa Ahmedabad, India.

"Tunatarajia mtaalamu huyo atafanya uchunguzi kuanzia tarehe 23, 24 na 25 Januari na wale watakaobainika kuwa na matatizo hayo watafanyiwa upasuaji," ilisema.

"Hii ni fursa ya kipekee kwa Watanzania wenye matatizo kama haya kuchangamkia fursa hii kwani badala ya kwenda nje na kutumia gharama kubwa kusafiri na wasaidizi wao kwenda nje ya nchi sasa wanafanyiwa upasuaji hapa hapa nchini."

# Kilimo cha umwagiliaji kupaisha uzalishaji chakula

**Na Mwandishi Wetu**, PEMBA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheri, amesema kilimo cha umwagiliaji kinaweza kuongeza uzalishaji na kuepisha uagizaji chakula kutoka nje ya Zanzibar.

Kheri aliyasema hayo katika bonde la mpunga Kwale Mpona Wilaya ya Wete alipokuwa akizindua mradi wa kilimo cha umwagiliaji. Waziri Haji aliwataka wakulima wa bonde hili kutunza mazingira ili kuhifadhi vyanzo vya maji ambayo ndio yanayosaidia kuendeleza mpango huo.

"Niwaombe wananchi wa maeneo jirani na wale wanaliomilikishwa kuitumia ardhi hii kwa kulima mazao katika bonde hili tusiwe na shauku ya kukata miti kila wakati," alieleza Waziri Haji.

Haji aliwataka wakulima hao kuwa makini sana na kutoa taarifa Idara ya Misitu pale wanapoona kuna uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo.

Pia aliwataka wakulima kuitunza miundombinu ya 'skimu' hiyo kwa kuweka usafi katika mitaro ili ichukue muda mrefu na kuwasaidia katika kuendeleza kilimo.

Akizungumzia suala la uzalishaji kwa mpango kwa skimu zote tisa, Waziri Haji alisema unatarajiwa kuzalisha kwa wastani wa tani 70,000 kwa mwaka.

"Baada ya kukamilika kwa mpango wa mradi huu, tunatarajia mavuno yatakuwa mazuri kwani wastani wa tani 70,000 zitazalishwa, hivyo huwenda tukapunguza gharama ya kuagiza mchele kutoka nje ya visiwa vyetu," alisema Waziri Haji.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Makame Ali Ussi, alieleza kuwa mradi huo ni kati ya miradi tisa (9) ambayo kama itatumika vilivyo itaweza kuzalisha tani 70,000 ambapo itaweza kupunguza uagizaji wa mchele kutoka nje ya nchi.

"Kwa mwaka wakulima katika bonde hili wataweza kulima mara mbili, hivyo itasaidia sana kuongeza kasi ya uzalishaji na pia pato kwa wakulima," alieleza Naibu Waziri.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kulima kwa kutumia njia za sasa na kutumia mbegu bora ili kuvuna mazao mengi na yenye ubora.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Omar Khamis Othman, alimhakikishia Waziri Haji kuwa watayafanyia kazi maagizo yote aliyoyatoa kwa lengo la kufanikisha mradi huo uweze kuleta maendeleo kwa jamii.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mansura Mosi Kassim, alisema kusudio la mradi huo ni kuongeza tija ya uzalishaji wa mpunga ili kuwe na chakula cha uhakika, na ziada na kuwaongezea pato wakulima na hatimaye taifa.

Mansura alieleza kuwa mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 671.7 na ujenzi wake ulianza rasmi mwishoni mwa mwaka 2018 na kukamilika mwishoni mwa mwaka jana.

HABARI KIMATAIFA

# Wafiwa ajali ya ndege kunufaika

**KYIV, Ukraine**

UKRAINE imetangaza kuwalipa fidia ya dola za Marekani 8,000 familia za raia wake waliokufa kwenye ajali ya ndege iliyotokea Iran mapema wiki hii.

Mpango huo umetangazwa na Rais wa nchi hiyo, Volodomyr Zelensky ambaye alisema atalazimisha pia Iran kutoa kiwango kingine cha fedha kitakacholipwa kama fidia kwa familia za wahanga hao.

Watu 176 wakiwamo raia 11 wa Ukraine walikufa wakati ndege ya shirika la Ukriane chapa Boeing 737 ilipoanguka muda mfupi baada ya kuruka kutoka uwanja wa ndege mjini Tehran.

Jana maofisa wa Iran walikiri ndege hiyo ilianguka baada ya kushambuliwa kwa bahati mbaya na kombora la Jeshi la Iran.

Rais Zelensky alizungumza kwa njia ya simu na Rais Hassan Rouhani wa Iran ambaye ameahidi nchi yake itawafungulia mashtaka wote waliosababisha kutokea ajali hiyo.

Wakati huohuo, maandamano makubwa yameripotiwa usiku wa Jumamosi kwenye maeneo kadhaa ya mji mkuu wa Iran Tehran, baada ya nchi hiyo kukiri kuwa kombora la kijeshi liliiangusha ndege ya abiria ya Ukraine.

Mamia ya wananchi walishiriki maandamano hayo ya usiku kuikosoa serikali ya nchi hiyo na hatua yake ya hapo kabla ya kupinga madai kuwa kombora lilikuwa chanzo cha ajali hiyo.

Kulingana na Shirika la Habari la Isna waandamanaji nje ya Chuo Kikuu cha Amir Kabir walitaka wote waliohusika na kuangushwa ndege hiyo wajiuzulu.

Naye Rais wa Marekani, Donald Trump, ameionya Iran dhidi ya kujaribu kufanya ukandamizaji wa maandamano hayo na kutoa wito kwa nchi hiyo kuruhusu makundi ya haki za kirai kufuatilia kile kinachoendelea.

Ujumbe wa Trump umekuja baada ya polisi kuwatawanya wanafunzi waliokuwa wakitoa kauli kali kuwakumbuka wahanga wa ajali ya ndege hiyo.

***DW***

## Rais wa zamani Ufaransa kufikishwa mahakamani

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa zamani wa Ufaransa, Nicolas Sarkozy, anatarajiwa kufikishwa mahakamani Oktoba, mwaka huu, kujibu mashtaka ya ufisadi.

Sarkozy anadaiwa kupokea taarifa muhimu kutoka kwa jaji kuhusu uchunguzi dhidi yake.

Atakuwa Rais wa kwanza wa Ufaransa kushtakiwa ndani ya miaka 60 kwa tuhuma za ufisadi katika taifa hilo la bara Ulaya.

Sarkozy anakabiliwa na tuhuma za kupokea pesa za kufadhili kampeni zake kutoka kwa kiongozi wa zamani wa Libya Kanali Muammar Gaddafi.

Mwaka 2013, Ufaransa ilianzisha uchunguzi kuhusu tuhuma kwamba kampeni ya Sarkozy ilipokea mchango kutoka kwa hazina ya pesa haramu za Gaddafi. Hata hivyo, Sarkozy amekanusha tuhuma hizo.

Novemba 2016, Ziad Takieddine alikiambia kituo cha habari cha Mediapart kuwa kati ya mwaka 2006-2007, alikabidhi mikoba mitatu iliyojaa noti za euro 200 na 500 kwa Sarkozy na mkuu wa watumishi wake, Claude Guéant.

Takieddine anadai pesa hizo zilitoka kwa Gaddafi na zilikuwa takriban Dola milioni 6.2 sawa na Euro milioni 5.

**RFI**



Rais wa Rwanda, Paul Kagame (kushoto), akiwa na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni. **PICHA: REUTERS**

## Djotodia arejea nyumbani baada miaka sita

**BANGUI, Afrika ya Kati**

RAIS wa zamani wa Jamhuri ya Afrika ya Kati, Michel Djotodia, aliyekuwa uhamishoni Benin tangu mwaka 2014, amerejea nchini juzi.

Djotodia, kiongozi wa zamani wa kundi la zamani la waasi la Seleka, alichukuwa madaraka mwaka 2013 baada ya kumpindua aliyekuwa wa Rais wa nchi hiyo, François Bozize.

Miaka sita baada ya kuondoka Bangui, Djotodia aliwasili jijini Bangui kwa ziara ya siku mbili.

Rais huyo wa zamani alikutana na familia yake mara tu alipowasili kabla ya kuelezea sababu za kurudi kwake.

"Nimekuja kutoa salamu zangu za mwaka mpya na kupendekeza kuwa ninaweza kuchangia ujenzi wa nchi. Nitakutana na Rais, nitamsikiliza, halafu tutaangalia jinsi ya kuweka mambo sawa. Sitokutana kwa mazungumzo na watu kwa sasa, mkutano wa wakuu wa zamani wa nchi, mawaziri wakuu wa zamani na viongozi wa vyama vya siasa, nadhani kuwa siku zijazo nitatakiwa kurejea nchini, " alisema Djotodia na kuongeza:

"Mimi si mtu wa vita tena, sasa ni mtu wa amani. Kwa hivyo nitawatoa hofu baadhi ya watu wenye mawazo kama hayo. Badala yake, nimekuja kusaidia wananchi wa Jamhuri ya Afrika ya Kati. inabidi raia hawa waishi kwa amani. Wamechoshwa na vita. Na hatutaruhusu mtu yeyote kuchukua silaha na kuwaangaisha kinamama, watoto na wazee nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati. Hatutaruhusu na hakuna tena waasi ambao wako msituni," alisema Djotodia.

Djotodia anatarajia kukutana na Rais Touadéra na wadau wote. Kuwasili kwake Bangui kunakuja wiki tatu tu baada ya Rais mwingine wa zamani François Bozizé kurejea nchini humo.

***RFI***

## Liberia yarejesha mifuko ya plastiki Ugiriki

**MONROVIA, Liberia**

MAMLAKA ya Liberia imesema kwamba imerejesha tani nne za mifuko ya plastiki nchini Ugiriki ni hatari kwa mazingira.

Mifuko hiyo ilikuwa imeingizwa nchini humo kimagendo kwa kisingizio kwamba inaweza kuchakatwa upya.

Mkuu wa Shirika la Kulinda Mazingira, Nathaniel Blama, alisema kuwa maofisa wa kupambana na bidhaa zinazoingizwa kimagendo nchini humo waligundua baada ya mzigo huo ulipowasili katika Bandari ya Monrovia ukiwa unanuka na kutoa harafu mbaya.

Aidha, uchunguzi umeanzishwa mara moja kuhusu namna mzigo huo ulivyoagizwa.

Baada ya kontena hizo kukaguliwa, shirika hilo limesema kuwa aina ya mifuko ya plastiki iliyoletwa, imepigwa marufuku kuchakatwa na kutumiwa tena nchini Ugiriki.

Maili 350 ya Pwani ya Liberia inalindwa na maofisa wa kushika doria na mara nyingi meli za uvuvi za kimataifa huingia eneo hilo kinyume cha sheria.

Mifuko ya plastiki imepigwa marufuku kutokana na uchafuzi wa mazingira duniani, na harakati za kukomesha matumizi yake yanalenga kulinda mazingira.

Hata hivyo, marufuku hiyo haihusishi vifungashio vya plastiki vya bidhaa mbalimbali.

Nchini Kenya mtu yoyote anayepatikana akitengeneza, kuuza au kutumia mifuko hiyo ya plastiki anaweza kupigwa faini ya hadi dola za Marekani 40,000 au kufungwa jela hadi miaka minne.

**BBC**

# DC ataka wadau kutetea wanawake

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, amewataka wadau wa haki na utetezi wa wanawake kuendeleza juhudi za serikali ili kuhakikisha wanawake wanalindwa dhidi ya ubaguzi wa aina yoyote na kushiriki katika fursa za maendeleo na ustawi wao.

Chonjo alisema hayo wakati wa kuahirisha kikao cha wadau wa kitaifa waliokutana mjini Morogoro kwa lengo la kuboresha taarifa ya nchi ya utekelezaji wa mkataba wa kimataifa wa kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake (CEDAW).

Mkuu huyo wa wilaya, aliwapongeza wadau kwa kuweza kuainisha mafanikio yaliyofikiwa na serikali katika kuzuia ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2019.

"Kazi hii ya kuandaa taarifa ya nchi ambayo mmeifanya kwa muda wa siku tatu itaboresha shughuli zilizofanyika na kuonyesha jinsi Tanzania ilivyotekeleza masuala ya kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake na pia kuwawezesha kiuchumi, kisiasa na kijamii," alisema.

Kwa mujibu wa Chonjo, idadi ya wanawake nchini ni kubwa ukilinganisha na idadi ya wanaume, huku akitaja takwimu zinaonyesha kuwa kuna takriban asilimia 51 ya wanawake ukilinganisha na wanaume na kati ya hao asilimia 80 wanaishi vijijini wakijiajiri katika shughuli za kilimo.

Aidha, alisema kuna umuhimu wa kuwalinda wanawake dhidi ya ubaguzi na aina zote za ukatili wa kijinsia ili kushiriki nafasi za maendeleo.

"Tukitambua kuwa idadi ya wanawake nchini ni kubwa kwa asilimia 51 ukilinganisha na idadi ya wanaume hoja hii inakuwa msingi wa kuwekeza katika kukuza ushiriki wa wanawake ambapo takriban asilimia 80 ya wanawake hao wanaishi vijijini wakiwa wamejiajiri katika sekta ya kilimo, hivyo kuna uhitaji mkubwa wa kupinga ubaguzi dhidi ya wanawake," alibainisha.

Alitaja hatua nyingine iliyochukuliwa na serikali kupunguza vitendo vya ukatili kuwa ni kufanya marekebisho ya Sheria ya Elimu na kulifanya kosa la kumpa mimba au kuoa au kuolewa mwanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuwa kosa la jinai na pale inapothibitika adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela, marekebisho haya yamesaidia kupunguza matukio ya mimba za utotoni.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Jinsia, Mboni Mgaza, alisema taarifa hiyo ya tisa, itawasilishwa Umoja wa Mataifa Machi 2020 ikiwa imeunganisha taarifa ya Tanzania Bara na Zanzibar.



Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Benki ya CRDB, Siaphoro Kishimbo, akizungumza na baadhi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, mkoani Morogoro wakati mkutano wa kuwapatia uzoefu wanafunzi hao wa namna ya kuitumia vyema elimu wanayoipata ili kukabiliana na soko la ajira, uliofanyika Januari 10, 2020 katika chuoni hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kanyasu aiagiza TFS kuanzisha vituo vya mbao

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameuagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuanzisha vituo maalum vya kuuzia mbao kama ilivyoanzisha maduka kwa ajili ya kuuzia asali.

Amesema kuanzishwa kwa vituo hivyo itakuwa ni hatua muhimu kwa TFS katika kuelekea kwenye uchumi wa viwanda kwa kuanza kuuza mbao badala ya magogo.

Kanyasu ameitaka TFS ianze kuchakata mbao zinazotoka kwenye misitu inayoisimamia, hali itakayosaidia kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato.

Mbali na kuanzisha maduka hayo ya mbao, Kanyasu ameitaka TFS ianze kufikiri kibiashara kwa mazao ya misitu inayoyazalisha kwa kuyaongezea thamani hali itakayopelekea kupata fedha zitakazotumika kwenye kuanzisha mashamba mapya ya miti ya kupandwa.

Alisema uamuzi huo wa TFS kuanza kuchakata na kuuza mbao zake utawasaidia walaji wa mwisho ambao ni wananchi kwa kuzinunua mbao hizo kwa bei nzuri ukilinganisha na mbao hizo kama zingeuzwa na wafanyabiashara ambao wananunua magogo ya miti kwa TFS.

Aidha, Kanyasu amesema hatua hiyo itaisaidia serikali kupata faida kubwa kwa kuuza bidhaa iliyoongezewa thamani, yaani mbao badala ya magogo.

Alisema uanzishwaji wa viwanda hivyo kutasaidia kuwadhibiti wafanyabiashara wadanganyifu wanaoshirikiana na maofisa misitu kukata miti ambayo ipo hatarini kutoweka.

Alifafanua kuwa katazo la serikali la kuzuia kukata na kusafirisha magogo ya miti migumu limechangiwa na TFS kwa sababu ya kutokuwa na viwanda vyake vyenyewe vya kuchakatia mbao.

Alifafanua kuwa TFS itakuwa na uwezo wa kuzalisha na kuuza mbao ngumu na mbao laini kwa wateja wake.

Alisema maduka hayo yataweza kuwahudumia wanunuzi wakubwa na wanunuzi wadogo wa mbao.

Akizungumzia uanzishwaji wa vituo hivyo maalum vya kuuzia mbao, Kanyasu alisema itakuwa suluhisho la kudumu kwa wananchi wanaolalamikia kuuziwa mbao changa kwa ajili ya ujenzi hali inayopelekea nyumba zilizojengwa kwa kutumia mbao changa kukosa uimara.

Alisema uamuzi huo utaisaidia TFS kuwa na vyanzo vya mapato vya kuaminika tofauti na ilivyo sasa ambapo imekuwa ikitegemea kwa kiasi kikubwa kukusanya mapato yake kwa kuwakamata wahalifu wanaosafirisha mazao ya misitu bila vibali.

Alisema chanzo hicho sio cha uhakika kwa vile ipo siku watu wakistaarabika na kuanza kufuatia sheria TFS itashindwa kujiendesha kwa kukosa mapato.

Katika hatua nyingine, Kanyasu ameipongeza TFS kwa kuanzisha maduka kwa ajili ya kuuza asali, ambapo kwa sasa jamii imekuwa na uhakika wa ubora wa asali inayoinunua katika maduka hayo.

Kufuatia hali hiyo, Kanyasu ameitaka TFS iharakishe taratibu za kupatiwa nembo kutoka Shirika la Viwango (TBS) ili asali hiyo iweze kuuzwa katika masoko ya kimataifa.

## RC afichua siri mafanikio kazini

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

BARAZA la wafanyakazi la Sekretarieti Mkoa wa Mtwara limeshauriwa kuongeza nguvu kuhakikisha linadumisha maelewano, ushirikiano na mshikamano kati ya wafanyakazi, uongozi na taasisi husika sehemu ya kazi ili kuweza kuleta tija kwa taifa.

Ushauri huo ulitolewa wilayani Masasi na Mkuu wa Mkoa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Baraza hilo mkoa.

Byakanwa alisema Baraza la Wafanyakazi lina wajibu wa kuhakikisha kunakuwapo na ushirikiano, maelewano, mshikamano katika sehemu ya kazi.

Alisema uwapo wa mshikamano na maelewano katika sehemu ya kazi kwa wafanyakazi kutasaidia kuongeza tija ya utendaji kazi jambo ambalo mwisho wa siku litaleta faida kubwa kwa taifa.

Byakanwa alisema moja ya siri kubwa katika kuleta mafanikio sehemu ya kazi ni kujenga umoja, uhusiano na maelewano tofauti na hapo hakuna mafanikio yeyote yatakayoletwa na mfanyakazi.

Alisema hakuna sababu kwa wafanyakazi kufanya kazi kwa misingi ya matabaka yao bali kuwapo na hali ya mshikamano na umoja.

"Hakikisheni mnadumisha ushirikiano na maelewano kwa wafanyakazi, uongozi na taasisi husika kwani hii itaondoa ufanyajikazi wa kitabaka na kuleta umoja kwa kila mfanyakazi," alisema Byakanwa.

Alisema iwapo kunakuwa na lugha moja ya maelewano kwa wafanyakazi, uongozi na taasisi husika sehemu ya kazi hata migogoro ambayo inayojitokeza kati ya wafanyakazi haitakuwapo kwa sababu wafanyakazi watakuwa kitu kimoja.

Byakanwa alisema Baraza la Wafanyakazi ndilo nyenzo kuu ya wafanyakazi, hivyo linalo wajibu wa kutatua changamoto za wafanyakazi na kuzifanyia kazi ili kujenga ushirikiano kazini.

Alisema baraza hilo pia lazima lihakikishe maslahi ya wafanyakazi ikiwamo kupata stahiki zao za upandishwaji wa madaraja wanapata.

**"Hakikisheni mnadumisha ushirikiano na maelewano kwa wafanyakazi, uongozi na taasisi husika kwani hii itaondoa ufanyajikazi wa kitabaka na kuleta umoja kwa kila mfanyakazi," alisema Byakanwa.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga 0758 112 332. Karibu EFL.

**WAHUDUMU WA HOTELI WANAHITAJIKA** Hoteli ndogo Bagamoyo inatafuta wahudumu, wapishi, usafi, bartender wenye vyeti. Kwa mawasiliano zaidi **Piga 0757 129 546.**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO


**TANGAZO KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI**

**ELENIA LUPONELO MHOKA** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari yake aina ya **TOYOTA HILUX-D/CABIN** yenye Namba za usajili T 280 ALV - Pick-up.

Chassis No. **LN1070000223.** Engine no **3L2784488.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

Taarifa Polisi MBI/RB/625/2019. Au piga simu namba 0757059933.

115581602


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# XAVI: KUINOA BARCA NI NDOTO YANGU

**BARCELONA, Hispania**

XAVI emeelezea kuwa kocha wa Barcelona ni "ndoto" yake, lakini akasisitiza kwamba anamheshimu kocha ambaye yupo kwenye presha kubwa, Ernesto Valverde.

Nafasi ya Valverde ipo kwenye sintofahamu katika kikosi hicho, baada ya Barca kukubali kipigo cha 3-2 kutoka kwa Atletico Madrid kwenye nusu fainali ya Kombe la Supercopa de Espana.

Kocha wa Al Sadd na gwiji wa Barca, Xavi amethibitisha ripoti kwamba amekutana na Mkurugenzi wa soka kutoka pale Camp Nou, Eric Abidal Qatar Ijumaa huku uvumi ukizagaa kwamba amepewa ofa ya kuchukua mikoba ya Valverde mwishoni mwa msimu huu.

Lakini Xavi mwenye umri wa miaka 39 hakutaka kuzungumzia kwa kina kuhusu mpango huo, akisisitiza kwamba anaiheshimu klabu yake hiyo ya zamani na kocha wake.

"Kuifundisha Barca ni ndoto yangu, siwezi kuficha hilo, kila mmoja anajua kwamba nawasapoti wao kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu," alisema Xavi akiwaambia waandishi wa habari baada ya kuiongoza Al Sadd kwenye fainali ya Qatar kwa ushindi dhidi ya Al Rayyan Jumamosi.

"Ndio, Abidal ni rafiki yangu. Nimekutana naye mara nyingi, hivyo siwezi kusema lolote, ni kwamba naiheshimu Barcelona, namheshimu Valverde, nawaheshimu wachezaji, naiheshimu klabu.

"Wao (Barca) walikuwa hapa kuzungumza na mimi na tulijadiliana mambo mengi."

## FIRMINO AOMBA RADHI KWA KUTOFUNGA MABAO MENGI

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema Roberto Firmino ameomba radhi kwa kutofunga zaidi wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Tottenham Jumamosi.

Matokeo hayo yanamaanisha kwamba wekundu hao wameshinda mechi 20 kati ya 21 kwenye Ligi Kuu msimu huu na wanaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu England kwa tofauti ya pointi 16 dhidi ya Leicester City iliyopo nafasi ya pili.

Firmino alifunga bao hilo pekee kwenye mchezo huo dakika ya 37 pale kwenye dimba la Tottenham Hotspur, lakini raia huyo wa Brazil alionekana kutoridhika na bao hilo, kwa mujibu wa kocha wake.

"Wakati nilipomfuata na kutaka kumkumbatia, alitaka kukataa na alitaka kwanza tuzungumze," alisema Klopp.

Alisema: "Najua nilitakiwa kufunga mabao mengi zaidi'. Lakini haikuwa kama nilivyotaka!

"Pengine ni kweli. Alitakiwa kufunga zaidi baada ya kupata nafasi kadhaa.

"Ni mchezaji mkubwa na nyota. Siwezi kusema hili kwa mara ya kwanza na nina matumaini sitasema kwa mara ya mwisho."




## SOLSKJAER AMSIFU GUARDIOLA KUIBADILISHA CITY

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema amesifia mbinu za mpinzani wake Pep Guardiola alivyoisuka Manchester City.

Kauli ya Solskjaer imekuja siku chache baada ya timu hizo kuvaana katika mchezo wa 'dabi' ya Manchester kwenye Uwanja wa Old Trafford katika nusu fainali ya kwanza ya Kombe la EFL.

Katika mchezo huo, City iliibuka na ushindi wa mabao 3-1.

Kabla ya mchezo huo United ilikuwa na kumbukumbu ya kuilaza City mabao 2-1 katika mchezo wa Ligi Kuu England.

Mchezo huo unarudisha nyuma miaka mitatu ambapo Manchester United ililaza Manchester City bao 1-0 lililofungwa na Juan Mata Oktoba 26, 2016 katika raundi ya nne kwenye uwanja huo.

Solskjaer mwenye umri wa miaka 46 alisema wachezaji wa Manchester City wanacheza kwa kiwango bora na siku zote wamekuwa na mchezo mzuri. Manchester City iliivaa Manchester United ikiwa mbele kwa pointi 13 katika Ligi Kuu England huku mahasimu wao wakishindwa kuonyesha kiwango bora tangu kuanza mwaka huu.

Manchester United ilicharazwa mabao 2-0 dhidi ya Arsenal kabla ya kucheza katika kiwango cha chini ilipotoka suluhu na Wolves ambapo haikupiga shuti langoni mwa wapinzani wao.

"Imekuja kivingine katika muda mwingine. Walipokuja wamiliki wapya, timu inacheza kwa kiwango bora. Inaendelea kuimarika na miongoni mwa klabu kubwa duniani," alisema kocha huyo.

"Kwa uhakika kabisa, City imebadilika kiuchezaji na Guardiola amefanya kazi nzuri, timu imekuwa na ushindani mkubwa zaidi na inaonyesha kuimarika kila siku," alisema.

## HABARI MICHEZO



# FERNANDES
## MBIONI KUONDOKA SPORTING

**LISBON, Ureno**

KOCHA wa Sporting Lisbon, Silas amekataa kuondoa uwezekano wa Bruno Fernandes kuondoka kwenye klabu hiyo ya Ureno wakati akiwa anahusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester United.

Nahodha huyo wa Sporting, Fernandes, ameripotiwa anakaribia kukamilisha uhamisho wa kwenda United baada ya klabu hizo mbili kudaiwa kufanya mazungumzo Ijumaa.

Fernandes alikuwa akihusishwa na mpango wa kwenda United, Tottenham na kwa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid mwanzoni mwa msimu huu, lakini uhamisho huo haukufanikiwa baada ya raia huyo wa Ureno kusaini mkataba mpya Novemba mwaka jana.

Baada ya kuifungia mabao mawili Sporting wakati ikiibuka na ushindi wa 3-1 kwenye Ligi Kuu Ureno dhidi ya Vitoria Setubal Jumamosi, Silas aliulizwa kama Fernandes tayari amefikia makubaliano na kama atakuwa kwenye mchezo dhidi ya Benfica.

"Siwezi kuwa na uhakika kuhusu hilo kwa sababu sijui," alisema Silas akiwaambia waandishi wa habari.

"Tayari nafikiria kuhusu mchezo wetu dhidi ya Benfica na nafikiria kuhusu kumtumia (Bruno Fernandes)."

Fernandes amefunga mabao nane na kutoa 'asisti' saba kwenye ligi msimu huu, huku akiwa amefunga mabao 15 kwenye mashindao yote.

***

# Van de Beek hataki kuondoka Ajax

**AMSTERDAM, Uholanzi**

NYOTA wa Ajax, Donny van de Beek amekataa kuondoka wakati huu wa usajili wa Januari huku akiwa anahusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester United na Real Madrid.

Van de Beek ameripotiwa kuwa anawaniwa na United, ambao wanataka kuimarisha safu yake ya kiungo huku Paul Pogba na Scott McTominay wakiwa majeruhi.

Miamba wa LaLiga, Madrid awali waliwasiliana na Ajax kuhusu uwezekano wa uhamisho huo, lakini dili hilo lilishindikana mwanzoni mwa msimu huu.

Licha ya kutakiwa sana, mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi, Van de Beek hana mpango wa kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, Ajax.

"Siwezi kufanya lolote kwa wakati huu," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 akiiambia FOX Sports.

"Nilishasema awali na nitasema tena: Nitabakia Ajax msimu huu. Na pengine msimu ujao.

"Habari hizi kuhusu Real Madrid au Man United sio nzuri, lakini sio muhimu kwa sasa. Nilisema nitabakia hapa Ajax na nitafanya hivyo kwa asilimia 100."



# CONTE: SIJUI CHOCHOTE KUHUSU VIDAL



**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte amekataa kuzungumzia kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa Barcelona, Arturo Vidal baada ya timu yake ya Inter Milan kutoka sare ya 1-1 nyumbani dhidi ya Atalanta kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Lautaro Martinez aliwapa bao mapema Nerazzurri hao kwenye dimba la San Siro, lakini Atalanta wakasawazisha kwenye mchezo huo uliopigwa juzi Jumamosi.

Robin Gosens alisawazisha dakika 15 kabla ya mchezo kumalizika na Samir Handanovic aliokoa penalti ya Luis Muriel kuiokoa Inter kupata kipigo cha pili msimu huu.

"Sizungumzii wachezaji ambao sio sehemu ya kikosi cha Inter," alisema Conte akiiambia DAZN wakati waandishi wa habari walipomuuliza kuhusu usajili wa Vidal.

"Niliingia kwenye mchezo huu bila ya wachezaji wanne muhimu. Atalanta ni timu ngumu, ikiwa na wachezaji wazuri.

"Tulifanya kila kitu tulivyoweza kutaka kushinda mchezo huu. Wachezaji walicheza vizuri.

"Leo (juzi) hatukuwa na Nicolo Barella, Matias Vecino kutokana na majeruhi. Najaribu kumrudisha Alexis Sanchez, kwa sasa tupo kwenye wakati mgumu."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MOURINHO AKIRI SPURS HAITASAJILI

Kocha huyo afunguka kuwatumia nyota waliopo ili kuziba mapengo ya majeruhi...

**LIVEROOL, England**

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amekanusha uvumi wa usajili unaowahusisha, Gedson Fernandes na Christian Eriksen.

Kiungo wa Benfica, Fernandes ameripotiwa kuwa anajiunga na Tottenham kwa mkataba wa mkopo wa miezi 18, huku nyota wa Spurs, Eriksen akitajwa kuwaniwa na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Inter Milan wakati huu wa dirisha la usajili mdogo wa Januari.

Huku mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, Eriksen amekuwa akihushwa na uhamisho wa kwenda Inter, ambao wamekanusha kuwasiliana na Tottenham.

Mourinho, hata hivyo hakutaka kuzungumzia kuhusu usajili wakati Tottenham wakifungwa 1-0 na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool juzi Jumamosi.

"Ni kitu cha mwisho nataka kufanya baada ya kiwango cha timu kwenye mchezo huu, kuzungumza kuhusu wachezaji wapya," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafikiri ni njia ya kuonyesha heshima kwa watu hawa ni kutozungumzia kuhusu wachezaji wapya.

"Tunaweza kusema (Japhet) Tanganga ni mchezaji mpya? Tunaweza kusema hivyo? Hakuichezea mechi yoyote Tottenham kwenye Ligi Kuu. Leo (juzi) ameichezea na amethibitisha kwamba anaweza kutuchezea vizuri.

"Uzuri kwamba yeye sio mshambuliaji, wala sio kiungo, lakini ni mmoja wa wachezaji tulionao.

"Hivyo nafikiri (Sadio) Mane na (Mohamed) Salah, wanamjua Tanganga ni nani. Hapo kabla ya mchezo hawakumjua. Wakati walipoona orodha ya wachezaji walishangaa huyu jamaa anacheza wapi. Nafikiri wanamjua sasa.

"Kijana kwa uhakika alikuwa vizuri, hivyo badala ya kumzungumzia Harry Kane na (Moussa) Sissoko na (Hugo) Lloris au Ben Davies, hebu tutabasamu kuhusu Tanganga."

Tottenham wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu na wakipitwa pointi nne na Chelsea waliopo nafasi ya nne kwenye msimamo baada ya kucheza mechi tatu bila ushindi.

## KWA UFUPI

**STONES HAKIJAELEWEKA**

HATIMA ya beki wa kati, John Stones katika kikosi cha Manchester City bado haijafahamika kufuatia mchezaji huyo kutofanya mazungumzo yoyote na klabu hiyo huku mkataba wa nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England ukibakiza miaka miwili. ***(Sunday Express)***

**FERNANDES AKARIBIA SPURS**

TOTTENHAM inajiandaa kuwazidi kete West Ham katika kuwania saini ya kiungo wa Benfica, Gedson Fernandes, ambaye ana umri wa miaka 21, na mkataba wake wa mkopo umebakiza miezi 18. ***(Sunday Mirror)***

**VAN DE BEEK ANUKIA UNITED**

KIUNGO wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Donny van de Beek, ametajwa kuhusishwa na tetesi za kutua Manchester United lakini nyota huyo bado hajafanya uamuzi wa kuondoka klabuni hapo katika dirisha dogo la Januari. ***(Fox Sports Netherlands, via ESPN)***

**WOLVES KUMNASA LEMAR**

WOLVES inaamini itafanikisha mchakato wa kumsajili winga wa Atletico Madrid, Thomas Lemar kwa sababu ya uhusiano mzuri walionao na wakala wa Mfaransa huyo, Jorge Mendes. ***(Mundo Deportivo, via Sport Witness)***

**ROJO SAFARI IMEIVA**

MANCHESTER United iko tayari kumtoa beki wake raia wa Argentina, Marcos Rojo (29), na kulipa ada ya pauni milioni 60 ili kufanikisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes, ambaye ana umri wa miaka 25 kutoka Sporting Lisbon. ***(Talksport)***

**SOUMARE MTEGONI**

MANCHESTER United inatarajia kwenda kumwangalia kwa mara ya mwisho kiungo wa Lille, Boubakary Soumare (20), kabla ya kuwasilisha ofa ya kumsajili nyota huyo wa kikosi cha Timu ya Taifa ya Vijana ya Ufaransa ya umri chini ya miaka 20. ***(Sunday Express)***

**KLOPP AMTAKA DEMBELE**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ameweka wazi nia ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(ElDesmarque - in Spanish)***

**WOOLFENDEN SOKONI**

MABOSI wa Sheffield United wanajiandaa kunasa saini ya beki wa kati wa Ipswich Town, Luke Woolfenden, baada ya klabu hiyo kuwa na mahitaji ya mabeki wawili wa kati. ***(Sheffield Star)***

**KADEWERE AGOMBEWA EPL**

ASTON Villa na Newcastle United zinajiandaa kuwania saini ya mshambuliaji Tino Kadewere katika dirisha dogo la Januari, huku Norwich City na Tottenham nazo zikionyesha nia ya kumsajili straika huyo wa Timu ya Taifa ya Zimbabwe mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

**WICKMAN KUONDOKA PALACE**

STRAIKA wa Crystal Palace, Connor Wickham (26), anajiandaa kutua kwa mkopo mabingwa wa Ligi ya Championship, Sheffield Wednesday kutokana na mshambuliaji wa Uturuki, Cenk Tosun (28), kutua hapo Selhurst Park. ***(Mail on Sunday)***

**ZLATAN ALIMVUTIA CONTE**

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte amesema alijaribu kusaka saini ya straika wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic (38), ambaye alitua Manchester United, wakati yeye alikuwa akiifundisha Chelsea. ***(Evening Standard)***

**BECKHAM, UNITED KUCHUANA**

MANCHESTER United itachuana na kiungo wake wa zamani, David Beckham ambaye anaimiliki Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu Marekani kuwania saini ya kiungo wa Boca Juniors na Argentina, Agustin Almendra (19). ***(Star on Sunday)***

HABARI MICHEZO

# KAKOLANYA AANIKA 'UCHAWI' WA KUCHEZA PENALTI ULIPO

**Na Isaac Kijoti, ZANZIBAR**

KIPA aliyetokea kukubalika zaidi kwa sasa na mashabiki wa Simba, Beno Kakolanya ameweka bayana siri kubwa katika kuicheza mikwaju ya penalti.

Katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Azam FC iliyopigwa Uwanja wa Amaan Ijumaa iliyopita, Kakolanya aliibuka shujaa wa Simba baada ya kuipeleka fainali.

Kakolanya alicheza penalti ya mwisho ya Azam iliyopigwa na kipa mwenzake Mghana Razack Abalora na kufanya Simba kutinga fainali ya michuano hiyo kwa penalti 3-2 baada ya matokeo ya suluhu ndani ya dakika 90.

Kwa matokeo hayo, Simba sasa itakutana na Mtibwa Sugar leo katika mechi ya fainali itakayopigwa Uwanja wa Amaan leo saa 2:15 usiku.

Akizungumza na Nipashe, Kakolanya alisema uchawi wa kucheza penalti ni kufanya mazoezi zaidi na hiyo ndiyo imekuwa siri ya mafanikio yake.

Kipa huyo alisema kwenye mazoezi amekuwa akifanyia kazi udakaji wa penalti na katika tano hucheza moja hadi mbili.

"Ninafanyia sana mazoezi udakaji wa penalti na nina uhakika kwa zaidi ya asilimia 90, huwezi kunifunga penalti zote tano, lazima nicheze moja ama mbili," alisema kipa huyo wa zamani wa Yanga.

Kwa sasa mashabiki wa Simba, wamekuwa wakipaza sauti zao kwa benchi la ufundi la klabu hiyo, wakitaka Kakolanya kuwa chaguo la kwanza kikosini dhidi ya Aishi Manula.

Kelele zilikuwa nyingi zaidi baada ya Manula kuruhusu mabao mawili kurudishwa kwenye Ligi Kuu dhidi ya Yanga wakati wakimaliza kwa sare ya 2-2, na wengi wakiamini ilitokana na makosa yake.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17, wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano maalumu ya Mercedes Benz Aegan yanayotarajiwa kufanyika nchini Uturuki kuanzia keshokutwa. **PICHA: TFF**

## Usajili Zanzibar hadi keshokutwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesogeza mbele dirisha dogo la usajili wa wachezaji na sasa litafungwa rasmi keshokutwa, badala ya Januari 9, kama ilivyotangazwa awali, imefahamika.

Kutokana na uamuzi huo, klabu zimeendelea kukamilisha mchakato huo kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao kuelekea mechi za Ligi Kuu Zanzibar itakayorejea tena kuanzia wiki ijayo.

Katibu wa Jang'ombe Boys, inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Dallas Abdallah, alisema kikosi chake kitasajili wachezaji wenye uwezo ili kuisaidia timu hiyo iweze kufanya vizuri katika ligi hiyo katika mzunguko huu wa lala salama.

Abdallah alisema Jang'ombe Boys haina malengo ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo msimu huu na inajipanga kufanya vizuri kwenye mechi zilizobakia ili isishuke daraja.

**"Kila timu inayocheza ligi ikiwa na malengo yake kufanya vizuri au kuwa bingwa, ila sisi ikitokea kama tutakuwa mabing wa tutafurahia ubingwa lakini tumejikita zaidi kuinusuru timu na janga la kushuka daraja, na hasa kumaliza katika nafasi tano za juu," alisema Abdallah.**

Kiongozi huyo alisema kuwa timu yake imewaacha wachezaji sita ambao wamesajiliwa na timu nyingine hivyo usajili wake utaangalia zaidi kuziba mapengo yaliyopo.

Aliwataja nyota waliachwa na kujiunga na timu nyingine ni pamoja na Abdallah Rashid, Ally Khamisi, Mohamed Haji, Simai Silima na Khalfan Abdallah.

Timu ya Jang'ombe Boys yenye pointi 13 ipo katika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu

# Matumla amtabiria makubwa Mtango

**Mwandishi Wetu**

BONDIA mkongwe nchini, Rashid Matumla amesema bondia, Salum Mtango, ana kiwango kizuri na anaamini ana nafasi ya kutwaa mkanda wa ubingwa wa dunia wa UBO dhidi ya mpinzani wake, Suriya Tatakhun kutoka Thailand.

Mabondia hao wanatarajia kukutana katika pambano la raundi 10 la uzani wa Light litakalofanyika Januari 31, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini, Tanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matumla alisema bondia wake alianza mazoezi mapema ili kujiandaa na pambano hilo na anaamini atapeperusha vizuri bendera ya Tanzania.

Matumla alisema hana wasiwasi na maandalizi ya Mtango, na anawaambia mashabiki wa ngumi kwamba mkanda wa pambano hilo utabaki nyumbani.

"Amekuwa akijifua kwa saa sita kila siku, anafanya mazoezi ya kujenga misuli, kutengeneza pumzi, programu hii itakwenda hadi siku mbili kabla ya pambano, anafanya pia mazoezi mepesi akisubiri kupanda ulingoni," alisema Matumla.

Alisema kwa ubora wa Mtango, anaamini ataibuka na ushindi wa Knock Out na hatamaliza raundi 10 zilizopangwa katika pambano hilo.

Mtango aliliambia gazeti hili kuwa amejiandaa kuweka historia ya kuwa bingwa wa dunia na kufuata nyayo za 'kaka' zake akiwamo Matumla ambaye sasa ni kocha wake.

"Nimefanya mazoezi kwa kiwango bora na bado naendelea kufanya mazoezi makali, nahitaji kuweka historia ya ubingwa tena kwa matokeo yasiyokuwa na utata, naamini nitashinda kwa KO," Mtango alisema.

Naye Mratibu wa pambano hilo, Ally Mwanzoa, alisema maandalizi yako katika hatua za mwisho na bondia Tatakhun anatarajiwa kuwasili nchini wiki moja kabla ya pambano.

Mwanzoa alisema kuwa mabondia wote watapima uzito na afya ifikapo Januari 30, mwaka huu jijini Tanga na zoezi hilo litakuwa la wazi.

Aliongeza kutakuwa na mapambano ya utangulizi ambapo bondia Mchanja Bakari atapigana na Sunday Kiwale kwenye uzito wa Light Fly wakati Saidi Mundi atachuana na Mustapha Dotto, huku Adam Yusuph akitarajiwa kucheza dhidi ya Bakari Mohamed, Idrissa Juma atapambana na John Ngotiko pia Mohammed Mutalemwa atazichapa na Simoni Buhura.

# Michezo

Jumatatu Januari 13, 2020

Nipashe




## Mourinho akiri Spurs haitasajili

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Tottenham Spurs, Japhet Tanganga katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku, Liverpool ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA: NI KOMBE TU

## Ni marudio ya fainali ya mwaka 2015, Katwila asema ni fainali ngumu ila Mtibwa Sugar itapambana, huku...

**Na Isaac Kijoti, ZANZIBAR**

TUNATAKA kombe la kwanza mwaka huu wa 2020, hiyo ndiyo kauli ya benchi la ufundi la Simba lililopo chini ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck akisaidiwa na mzawa, Selemani Matola.

Simba na Mtibwa Sugar inayonolewa na Zuberi Katwila, zitashuka katika dimba la Amaan leo kwenye mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Mechi hiyo inayotarajiwa kupigwa kuanzia saa 2:15 usiku ni kama marudio ya fainali ya mwaka 2015 timu hizo zilipokutana na Simba kutwaa ubingwa kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Mtibwa Sugar inashuka dimbani baada ya kuitoa Chipukizi kwa mikwaju ya penalti 4-2 katika hatua ya mtoano kufuatia sare ya bao 1-1 na kisha nusu fainali kuitupa nje Yanga kwa idadi hiyo ya penalti kutokana na sare ya 1-1.

Simba yenyewe, hatua ya mtoano iliichapa Zimamoto mabao 3-1 kisha nusu fainali ikaitoa Azam FC kwa penalti 3-2 kufuatia dakika 90 kumalizika kwa sare tasa.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven amesema utakuwa mchezo mgumu kwa timu hizo zinazotoka Ligi Kuu Bara kukutana leo, lakini wamejiandaa vema na wanachotaka ni kombe la kwanza mwaka huu.

Aliliambia Nipashe kuwa Mtibwa Sugar ni timu nzuri na inacheza soka la kuvutia, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu kwao kukata tamaa.

"Mechi ya fainali hakuna timu ndogo na Mtibwa wanacheza vizuri, ila tunachotaka ni kombe," alisema.

Mbelgiji huyo alisema anashukuru katika mechi zilizopita hakukujitokeza majeruhi jambo ambalo linampa wigo mpana wa kupanga kikosi chake.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Katwila, akiwa na kumbukumbu ya kulibeba kombe hilo wakati akiwa mchezaji wa timu hiyo mwaka 2010, alisema anafahamu Simba ni timu bora na wamejipanga kwa hilo.

Katwila alisema ukishafika fainali utarajie kukutana na timu bora, lakini si hilo tu anatambua ubora wa Simba mwaka huu hivyo itakuwa mechi ngumu.

"Tumekuja kupambana na tunataka kombe ingawa tunajua mechi itakuwa ngumu kwa kila upande," alisema kocha huyo ambaye mwaka 2010 akiwa mchezaji walilitwaa kombe hilo kwa kuifunga Ocean View katika mchezo wa fainali.

Bingwa wa michuano hiyo mbali na kombe na medali za dhahabu atajinyakulia Sh. milioni 15, huku mshindi wa pili akilamba Sh. milioni 10 na medali za fedha.

# Tanzania mwenyeji Kombe la Kagame

**Na Somoe Ng'itu**

MASHINDANO ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame mwaka huu yamepangwa kufanyika jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Simba ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Yanga ilimaliza katika nafasi ya pili msimu uliopita wana nafasi ya kushiriki mashindano hayo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye, alisema uamuzi huo umepitishwa rasmi katika mkutano mkuu wa baraza hilo uliofanyika Desemba mwaka jana.

Musonye ambaye ataachia ngazi nafasi hiyo baadaye mwaka huu alisema mashindano ya Kombe la Chalenji yatafanyika Sudan wakati ya wanawake yatacheza Rwanda pamoja na michuano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za vijana za wasichana za umri chini ya miaka 17 kwa ukanda huu.

Alisema mashindano ya wanawake ya umri chini ya miaka 20 yatafanyika Uganda wakati yale ya wavulana ya umri chini ya miaka 16 yakipelekwa Djiboiti na Burundi itakuwa mwenyeji wa michuano ya wavulana ya U-20 pamoja na U-17 wasichana.

Aliongeza kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya Cecafa iliyoko chini ya Rais wa baraza hilo, Wallace Karia, iliteua Kamati ya Mashindano ya watu watano ambao watafanya kazi kwa kushirikiana na Ofisa Mtendaji Mkuu atakayekuja ili kufanya majukumu ya kila siku.

Alimtaja Mwenyekiti wa kamati hiyo atakuwa ni Doris Petra kutoka Kenya na wajumbe wake ni Aimable Habimana (Burundi), Bani Ahmed (Sudan), Justus Mugisha (Uganda) na Eunice Ali wa Djibouti.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >